## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

## MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**MEI, 2022**

# YALIYOMO

A. UTANGULIZI ........................................................... 1
B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YAHABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI 2021/2022 ............................ 5
C. UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MAPATO........................................ 6
D. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PRGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022 .............................. 7
E. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.......................................................... 60
F. MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.................................... 61
G. PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023......... 63
H. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 .................................................. 71
I. HITIMISHO ........................................................... 73
VIAMBATANISHO ........................................................ 77

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO, MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza tunao wajibu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kuwa hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu atupe umri mrefu na Afya yenye siha, na azidi kuibariki nchi yetu, aijaalie amani na utulivu.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nampongeza **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa namna anavyotuongoza na kutekeleza mabadiliko makubwa kwa wananchi wa

Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie uzima na Afya njema ili aweze kukamilisha azma yake ya kuleta maendeleo katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, amekuwa kiongozi wa mfano kwa kuwa karibu na Viongozi, Watendaji na Wananchi. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara katika uongozi wake.

5. **Mheshimiwa Spika,** nachukuwa nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Othman Masoud Othman,** Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo anaendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika majukumu yake ya kila siku ya kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika,** pongezi maalum nazitoa kwa **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar** kwa namna ambavyo anaendelea kumsaidia **Mheshimiwa Rais** katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kuongoza, kusimamia na kufuatilia shughuli za Serikali katika kipindi cha awamu ya nane.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nakupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza vyema Baraza hili tukufu kwa kutumia hekima, busara na weledi wa hali ya juu. Pia, nampongeza **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma** Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, yeye ni mwanamama jasiri na mchapa kazi na kwa hakika ni kigezo tosha kwa wanawake wote.

8. **Mheshimiwa Spika,** pongezi maalum nazipeleka kwa kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Mohammed Ahmada Salum** pamoja na Makamo Mwenyekiti **Mheshimiwa Mwantatu Mbaraka Khamis** kwa kuiongoza vyema kamati hii kwa hekima, busara, weledi, pamoja na Waheshimiwa wajumbe wote wa kamati kwa ushirikiano, ushauri na nasaha wanazotupatia kwa kutuongoza vyema katika kufanikisha malengo ya Wizara hii.

9. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kuwapongeza Wenyeviti, Makamo Wenyeviti na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Bajeti na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC).kwa maelekezo wanayotupatia ambapo Wizara yangu inafarajika sana na ushauri na maelekezo tunayopata kutoka kwa Kamati, nasema ahsanteni sana.

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imeundwa na Sekta Kuu nne nazo ni **Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo** zinazosimamiwa na taasisi **17** kama zifuatazo:-

i. Idara ya Utumishi na Uendeshaji;
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
iii. Ofisi Kuu Pemba;
iv. Idara ya Habari Maelezo;
v. Shirika la Utangazaji Zanzibar;
vi. Shirika la Magazeti ya Serikali;
vii. Tume ya Utangazaji;
viii. Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMUX);
ix. Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar;
x. Idara ya Maendeleo ya Vijana;
xi. Baraza la Vijana Zanzibar;
xii. Idara ya Utamaduni na Sanaa;
xiii. Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA);
xiv. Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU);
xv. Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (COSOZA);
xvi. Idara ya Michezo; na
xvii. Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ).

11. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba uniruhusu niwasilishe Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Habari, Vijana,

Utamaduni na Michezo kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022.

## B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI 2021/2022

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imeweza kutekeleza Programu kuu nne (4) na Programu ndogo nane (8) chini ya Fungu J03. Programu Kuu ni hizi zifuatazo:
    i. Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji;
    ii. Programu ya Maendeleo ya Vijana;
    iii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
    iv. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

13. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hizi umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (Zanzibar Development Vision 2050) pamoja na Mkakati wa Maendeleo ya Muda wa Kati Zanzibar (2021/2026).

## C. UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MAPATO

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 70,893,081,000/=** katika fungu la J03. Kati ya fedha hizo **Shilingi 14,424,100,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 56,468,981,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2022, jumla ya **Shilingi 8,706,893,417/=** sawa na asilimia **12** ya bajeti yote zimepatikana. Katika fedha za Matumizi ya Kazi za kawaida **Shilingi 7,917,893,415/=** sawa na asilimia **55** zimepatikana na katika fedha za miradi ya Maendeleo **Shilingi 789,000,000/=** sawa na asilimia **1** zimepatikana. **Kiambatanisho Namba 1A kinahusika.**

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 9,458,956,890/=**. Kati ya hizo, **Shilingi 1,134,200,000/=** ni makusanyo yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, **Shilingi 8,074,730,890/=** ni mapato yanayokusanywa na kutumiwa na taasisi na **Shilingi 250,026,000/=** ni makusanyo ya mirabaha. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 makusanyo halisi ni **Shilingi 4,454,565,295/=.** Kati ya hizo **Shilingi 464,755,419/=** sawa na asilimia **34** ni makusanyo yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa

Serikali, **Shilingi 3,989,809,876/=** sawa na asilimia **49** ni makusanyo yanayotumiwa na Taasisi na **Shilingi 100,487,394/=** sawa na asilimia **44** ni makusanyo ya mirabaha. **(Kiambatanisho namba 1B, 1C na 1E vinahusika)**

## D. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PRGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### i. Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji

16. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inaundwa na programu ndogo mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji.

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 50,119,606,000/=** kati ya hizo **Shilingi 4,553,225,000/=** ni mishahara na **Shilingi 3,097,400,000/=** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 42,468,981,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

18. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, jumla ya **Shilingi 4,641,780,485/=** sawa na asilimia 9 zilipatikana kati ya hizo, **Shilingi 3,376,909,485/=** sawa na asilimia 74 ni mishahara, **Shilingi 596,871,000/=**

ni matumizi mengineyo sawa na asilimia **19** na **Shilingi 668,000,000/=** sawa na asilimia **2** za Miradi ya Maendeleo.

**Programu Ndogo 1: Upatikanaji na Usambazaji wa Habari**

**19.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) na Kampuni ya Unganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX). Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 25,324,165,000/=.** Kati ya hizo **Shilingi 6,122,665,000/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 19,201,500,000/=** kwa Miradi ya Maendeleo.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **Shilingi 3,494,866,550/=** sawa na asilimia 14 zilipatikana. Kati ya hizo **Shilingi 2,826,866,550/=** sawa na asilimia 46 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 668,000,000/=** sawa na asilimia **3** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D).**

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari Maelezo iliwasilisha Waraka Serikalini wa kuwatambua na

kuwasimamia Maafisa Habari na Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ukweli na uhakika. Katika kutekeleza dhamira hii , Idara kwa kushirikiana na Idara ya Utumishi Serikalini imekamilisha Muundo wa Maafisa Habari sambamba na kufanya uhakiki wa Maafisa hao kwa lengo la kuwa na taarifa za pamoja **'database'.** Jitihada hizo zinalenga kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapatiwa taarifa sahihi za Serikali na kwa wakati muafaka kuhusiana na utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali na pia kuwa na uratibu mzuri wa kutoa habari za Serikali. Aidha, Idara iliratibu mafunzo ya siku 5 kwa Maafisa Habari na Mawasiliano 12 wa Serikali yaliyoandaliwa na Chama cha Maafisa Habari na Mawasiliano wa Tanzania (TAJCO) yaliyofanyika Jijini Dodoma mwezi wa Januari 2022.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kusambaza taarifa za kihabari **928** za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni zikiwemo ziara na mikutano ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na viongozi wa Serikali, kuapishwa kwa viongozi walioteuliwa, uzinduzi wa miradi ya maendeleo, mikutano ya waandishi wa habari na maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Aidha, taarifa za matukio tofauti ya Kiserikali zimechapishwa kwa njia ya picha na kuekwa kwenye mabango na kusambazwa kwenye maeneo tofauti ya Wilaya nne

za Pemba. Aidha, taarifa za kihabari ziliandikwa na kusambazwa kwenye vituo mbali mbali vya habari kama vile ZBC redio, ZBC Tv, Chuchu Fm Redio, Redio Istiqama, redio Jamii Micheweni na Tumbatu pamoja na Shirika la Magazeti ya Serikali. Taarifa hizo zilioneshwa kwenye bango la kielektroniki **"Display Board"** lililopo eneo la Kisonge, samabamba na kuweka taarifa kwenye mitandao ya kijamii ili wananchi walio wengi waweze kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusiana na matukio mbali mbali yanayojiri nchini.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Idara imeweza kuuza nakala za picha **712** za Viongozi Wakuu wa nchi zikiwemo picha **93** za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, picha **502** za Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya sita, picha **69** za Rais Wastaafu na picha **48** za Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari Maelezo imeweza kuonesha sinema kuhusiana na dhana ya Uchumi wa Buluu katika vipengele vya Ukulima wa Mwani, Ufugaji na Uvunaji wa Majongoo. Kwa hatua ya awali jumla ya vijiji (8) vimefikiwa ikiwa ni pamoja na Matemwe Gomani, Mangapwani, Pongwe Pwani, Michamvi, Marumbi, Kiwengwa na Pwani Mchangani. Pia Idara imeweza kushiriki katika kuadika historia ya Miaka 58 ya Muungano.

25. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati, Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) limeweza kuandaa na kurusha hewani vipindi na matangazo kupitia TV na Redio pamoja na mitandao ya kijamii. Jumla ya vipindi vya ndani **8,753** vimerushwa hewani, vikiwemo Ukweli si uvumi, Chowea, Zanzibar Wiki hii, ZBC Dokta, Ajira ni Biashara na Muelekeo wetu. Aidha, vipindi vyengine vilivyorushwa hewani ni pamoja na vipindi vya Watoto na Burudani, Michezo na Maigizo, makala na habari kutoka katika channel mbalimbali za nje.

26. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) limefanikiwa kurusha hewani vipindi **14,156** vya ZBC Redio na Spice FM vikiwemo vipindi vya ziara za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar pamoja na Viongozi Wakuu wa Serikali, vipindi vya miaka **58** ya Mapinduzi ya Zanzibar, Vipindi vya uchambuzi wa maagizo **13** ya **Mheshimiwa Raisi,** kwa Mawaziri na vipindi vya kawaida vikiwemo kutoka jimboni, Mazungumzo ya asubuhi, Mawio, Badilika, Thamani yangu, Afrika yetu, Tungo zetu, Vijana, Utalii wa ndani, Michezo, Sauti yao na Weekend special.

27. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) limeweza kurusha matangazo ya moja kwa moja (live) 175, ikiwemo Maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi,

Kuapishwa kwa viongozi walioteuliwa, Uzinduzi wa Mwenge wa Uhuru Kitaifa na ufunguzi na uwekaji wa mawe ya msingi ya miradi ya maendeleo nchini. Aidha, jumla ya matangazo 16,547 yamerushwa hewani kupitia Redio na TV yakiwemo matangazo ya vifo, matangazo maalumu na matangazo ya biashara.

28. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) limefanikiwa kuanzisha vipindi vipya vikiwemo Kurunzi ya ZBC, Asili zetu, Usiku wa zilipendwa, Nuru ya Quran kwa upande wa Redio na vipindi vya Rahatu Zaman, Shani ya Mola, Mashindano ya Qur-an, Urithi wetu na Maisha kwa upande wa TV. Sambamba na hilo, ZBC katika kutimiza mwaka mmoja wa **Dk. Hussein Ali Mwinyi** pamoja na kusherehekea miaka 58 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ilirusha hewani vipindi vya moja kwa moja kwa Waheshimiwa Mawaziri wote katika kuelezea mafanikio na utekelezaji wa majukumu ya mawizara yao. Waandishi wa habari walipata fursa ya kuuliza masuali ya papo kwa papo na kupatiwa majibu ya Serikali.

29. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) linaendelea na kutekeleza jukumu lake la msingi la kuchapisha Gazeti la kila siku la Zanzibar Leo, Magazeti ya kila wiki Zanzibar Mail, Zanzibar Leo Jumapili, Zaspoti na Gazeti la kila mwezi Zanzibar Leo Wanawake na kuyasambaza katika Mikoa yote

ya Zanzibar pamoja na mikoa 11 ya Tanzania Bara. Lengo ni kutoa habari, kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa pamoja na kutangaza sera, mikakati na mipango ya Serikali. Pia, kutoa burudani na taarifa za michezo.

30. **Mheshimiwa Spika,** Shirika lilipanga kuchapisha nakala **1,482,000** kwa magazeti yake yote na limefanikiwa kuchapisha jumla ya nakala **927,000** sawa na asilimia **63** mpaka Machi 2022. Kwa upande wa matangazo, Shirika lilipanga kutoa matangazo **1,700** na kufanikiwa kutoa matangazo **1,032** sawa na asilimia **61**. Kupungua kwa kiwango cha matangazo kunatokana na uhaba wa fedha kwa taasisi mbali mbali na ushindani mkubwa wa kibiashara katika Sekta ya habari.

31. **Mheshimiwa Spika,** Shirika liliadhimisha miaka **20** ya kuanzishwa Gazeti la Zanzibar Leo na limefanikiwa kubadilisha muonekano wa Gazeti la Zanzibar Leo na Zanzibar Leo Jumapili na kuimarisha mitandao yake ya kijamii pamoja na kuanzisha tovuti mpya ili kuendana na matakwa ya sasa. Aidha, Shirika linaendelea na jitihada za kuimarisha magazeti mengine ya Zanzibar Mail na Zaspoti ambapo kupitia maboresho haya yatapelekea kuongezeka nakala kutoka **1,482,000** hadi **1,485,500** kwa mwaka. Vile vile, Shirika linauza magazeti kwa njia ya Mtandao (*E-Paper*) ili kuwapatia

fursa watu wengi ndani na nje ya nchi na kuchangamkia fursa za matangazo mtandaoni (*Digital marketing and Advertisements*). Shirika limejipanga kuongeza maeneo ya usambazaji magazeti kutoka Mikoa **11** hadi **16**, mawakala kutoka **10** hadi **18** Tanzania Bara. Katika kujitangaza shirika limefanikiwa kusambaza kurasa za mbele na nyuma kwenye blogsports **8** na gazeti la ZanzibarLeo linasomwa katika Televisheni **6** Tanzania ikiwemo ZBCTV, TBC,CHANNEL TENA, AZAM TV, CLOUDS TV na StarTV

**32.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Bodi na Menejimenti ya Shirika kwa mabadiliko makubwa sana yanayoendelea. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. Pia naomba kutoa wito kwa watendaji wa Serikali na wananchi kwa ujumla kuendelea kuyatumia magazeti yanayozalishwa na Shirika hili kwa kuyasoma, kupata taarifa mbali mbali za habari na matukio, na pia kutangaza biashara zao ili shughuli zake ziweze kuimarika na kutoa tija inayotarajiwa na Serikali.

**33.** **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMUX) imefanikiwa kuundwa kwa bodi kwa mujibu wa Sheria, jambo ambalo halikuwepo tokea kuanziswa kwake. Pia, kampuni imepata Mkurugenzi Mtendaji aliyeteuliwa na **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa**

**Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.** Katika hatua nyengine, Kama nilivyoahidi katika Baraza hili tukufu kuwa ZMUX itairejesha chaneli inayopendwa na wanachi ya **Mambo TV,** ambayo sasa kuna chaneli mbili zinazotokana na Mambo TV ambazo ni "Mambo Swahili" na **"Mambo Moto"** pamoja na kuanzisha chaneli nyengine mpya za **"ZMUX TAQWA"** na **"ZMUX MOVIES"** ambazo uzinduzi wake umeanza mwezi mosi Ramdhani ya mwaka huu wa 2022. Hii ni miongoni mwa mikakati ya kuingia kwenye soko la ushidani na kujiendesha kibiashara.

**34.** **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, kampuni imefanikiwa kufanya kampeni ya kujitangaza na kutoa elimu ya nyumba kwa nyumba katika Mikoa mitano ya Zanzibar. Lengo ni kuwajuilisha wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na Kampuni na kuwahamasisha kutumia ving'amuzi vya ZMUX. Hali hii imesaidia kuongeza wastani wa watazamaji kutoka **25,000** hadi **29,000** kwa mwezi.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uunganishaji Maudhui (ZMUX) imefanikiwa kutengeneza Mpango wa Biashara (*Business Plan*) kwa lengo la kuhakikisha Kampuni itajiendesha kibiashara na hatimae kuweza kutoa gawio Serikalini. Katika kuunga mkono juhudi za Serikali kuinua michezo, Kampuni imechangia

udhamini wa Ligi Kuu ya Zanzibar pamoja na kutengeneza mabango sita ya matangazo ambayo yamewekwa katika viwanja vya Amaan, Mao Ze Dong na Gombani.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uunganishaji Maudhui (ZMUX) imefanikiwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo vya kurushia maudhui pamoja na kuvipatia huduma ya umeme na mafuta kwa ajili ya majenereta ili kuhakikisha huduma zinapatikana muda wote. Vituo hivyo ni Masingini, Nugwi na Muyuni kwa Unguja na Kichunjuu, Chake Chake na Bungala kwa Pemba. Wahandisi wa Kampuni na Wakala wa Mkonga wa Taifa (ZICTA) wanashirikiana vyema kutatua changamoto za minara. Sambamba na hayo, wahandisi watano walisafiri kwenda Dar es Salaam kujifunza na kupata uzoefu kupitia Kampuni za Azam Media, Star Times na DSTV. Kampuni inaendelea kutatua changamato za mitambo iliyopo Pemba na vifaa vipya vimeshawasili kwa ajili ya kufanya marekebisho yanayotakiwa.

**Mradi wa Uimarishaji Utoaji wa Matangazo ZBC**

37. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uimarishaji Utoaji wa Matangazo ZBC unatekelezwa katika Programu ndogo ya Upatikanaji na Utoaji wa Habari. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mradi huu ulipangiwa jumla ya

**Shilingi 19,091,163,948/=** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kurushia matangazo. Hadi kufikia mwezi Machi 2022, Mradi haukuingiziwa fedha.

**38.** **Mheshimiwa Spika,** aidha, katika mradi huu fedha zilizopatikana ni kwa ajili ya Mradi wa Ununuzi Wa Vifaa Vya Studio, Samani Za Ofisi, Vifaa Vya Kompyuta na UPS (Uncorrupted Power Supply) ambazo ni jumla ya **Shilingi 668,000,000/=** zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 na kupatikana katika mwaka wa fedha 2021/2022.

**Programu ndogo 2: Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

**39.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Tume ya Utangazaji Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.

**40.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shillingi 24,795,441,000/=** ambapo **Shilingi 1,527,960,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 23,267,481,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya **Shilingi 1,146,913,935/=** sawa na asilimia **5** zimepatikana kwa ajili ya matumizi ya

kazi za kawaida na hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D).**

41. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutoa vibali **23** vya uchukuaji wa picha za kutengenezea filamu kwa makampuni tofauti. Miongoni mwa makampuni hayo ni pamoja na Peter Greenberg Worldwide na Blue Print Production, ambao walitengeneza filamu fupi ya Royal Tour iliyowashirikisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Gambi Teaser kutoka Ufaransa, TV2 kutoka Denmark, Buccaneer Diving kutoka Zanzibar, Film Fixer, Africa, Baker & Co Production, Chick Flick Movie, Film Fixers kutoka South Africa na kadhalika.

42. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari maelezo imesajili vijarida vitatu **(3)** ambavyo ni uchumi wa buluu kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, makamo wa Kwanza Kutoka ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Public policy kutoka *Zanzibar Institute for Research and Public Policy*. Katika hatua ya kudhibiti, kusimamia na kuwawezesha waandishi wa habari waliopo nchini kufanya kazi zao bila ya vikwazo Idara imefanikiwa kutoa vitambulisho **141** vya waandishi wa habari wanaofanya kazi katika vituo vya utangazaji na magazeti mbalimbali hapa nchini.

43. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utangazaji Zanzibar imefanikiwa kutoa jumla ya leseni **13** za vituo vya utangazaji vikiwemo redio **6**, televisheni **4** na maudhui ya mitandaoni **3**. Kati ya leseni hizo, redio ni DIZZIM Fm, Kati Fm, Bomba Fm, AM **24**, Mtegani Fm, na Zenj Fm, kwa upande wa televisheni ni Haiba TV, Zanzibar Joy TV, Zanzibar Joy Gospel na KMEC TV na kwa upande wa vituo vya maudhui ya mitandao ni *"Wor'out"* Media, Mshindo online TV na Pena online TV. Aidha Tume imefanikiwa kuvifuatilia na kurikodi matangazo ya vituo **18** vya redio za FM.

44. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utangazaji Zanzibar imetafsiri kanuni ya Utoaji Leseni za Utangazaji ya mwaka 2020 kwa Lugha ya Kiswahili na kwa sasa kanuni hizo zipo katika hatua ya kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Aidha, Tume imefanikiwa kufanya vikao vitatu vya bodi na mikutano minne na wadau wa Utangazaji nchini. Mikutano hiyo ilihusu ulipaji wa ada za leseni na kufuata maadili ya Utangazaji pamoja na kujadili mikakati ya kuiendeleza tasnia ya Utangazaji. Matokeo ya Mikutano hiyo ni kuwepo kwa ongezeko la kulipa ada na pia kufuata kanuni za utangazaji. Tume imetoa tangazo rasmi kwenye vyombo vya Habari la kuchukuwa hatua kwa mujibu wa kanuni kwa vituo vilivyokiuka masharti ya leseni zao.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira bora ya kazi Tume ya Utangazaji Zanzibar imeipatia Ofisi vifaa vya kuandikia, mafuta ya petroli, malipo ya umeme na maji. Aidha, wafanyakazi saba (7) wamepatiwa mafunzo ya awali kazini (induction course), kulipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo likizo (5) na muda wa ziada (5).

46. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar imefanikiwa kuchapisha nyaraka na taarifa **147** za Serikali Kuu zinazowasilishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nyaraka hizo ni Sheria, Kanuni, Miswada ya Sheria na Magazeti rasmi ya Serikali. Mpaka Machi 2022, Wakala imepokea jumla ya kazi 904 za uchapaji zenye thamani ya **Shilingi 929,642,490/=**. Kati ya hizo, kazi **821** zimekamilika na kazi **83** zinaendelea kuchapishwa. Pia, kati ya kazi hizo, **752** kutoka katika Taasisi za Serikali na **207** za taasisi binafsi.

47. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji inaendelea kutoa huduma za Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisi na kuandikia. Wakala umepokea bidhaa za Bohari Kuu mnamo tarehe 21 Febuari, 2022 na 31 Machi, 2022, na tayari bidhaa hizo zipo katika ghala. Aidha, Jumla ya maombi ya huduma ya vifaa vya ofisi na vya kuandikia kutoka katika Taasisi **46** za Serikali yamepokelewa. Kati ya Taasisi hizo, **37** zimepatiwa

vifaa vyote vilivyohitajika na Taasisi **9** taratibu za upelekaji wa bidhaa zinaendelea kufanyika. Pia, Wakala imefanikiwa kukodi ghala katika eneo la Kwahani la kuweka vifaa vyake hasa vile vya kiofisi ili kuimarisha ufanisi wa kazi zake.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji ulipokea maombi ya uchapishaji wa kazi ya mitihani kutoka Baraza la Mitihani la Zanzibar. Wakala umefanikiwa kuchapisha kazi hiyo ya Mitihani ya Darasa la Nne, Darasa la sita na Kidato cha Pili kwa wakati, ufanisi na kwa usiri mkubwa.

**49.** **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Wakala imeanza kuchapisha madaftari na kusambaza kwa wafanyabiashara na Skuli binafsi. Jumla madaftari **16,200** yamezalishwa na kuuzwa. Aidha, wakala unaendelea kuimarisha mitambo yake ya uchapaji na jumla ya mitambo **14** imefanyiwa matengelezo madogo na mitambo **3** matengenezo makubwa kwa kutumia mafundi wa ndani na hivyo kuokoa fedha nyingi za Serikali.

**Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji**

**50.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa chini ya programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya

Habari, Utangazaji na Uchapaji. Kwa mwaka wa fedha 2021/22 ulipangiwa kutumia **Shilingi 9,520,000,000/=** kwa ajili ya ununuzi wa mitambo nane (8) ya kisasa ya uchapaji. Hadi kufikia Machi 2022, mradi huu haujaingiziwa fedha.

**Mradi wa Ununuzi wa Mtambo wa kuchapisha Magazeti**

51. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lako Tukufu liliidhinisha Mradi huu kuhamishwa kutoka Shirika la Magazeti ya Serikali na kupelekwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2021/22 Mradi huu ulipangiwa kutumia **Shilingi 13,747,481,000/=** na hadi kufikia Machi 2022 mradi huu haujaingiziwa fedha.

52. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Serikali wa Uchapaji tayari imeshapata aina na sifa za mitambo (*technical specification*) inayohitajika na imeshaandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuwapatia wasambazaji wa mitambo hiyo. Aidha, Wakala wanaendelea na mchakato wa ujenzi wa jengo Maruhubi litakalotumika kwa ajili ya kuweka mitambo hiyo.

### ii. Programu ya Maendeleo ya Vijana

53. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 7,538,121,000/=** kati ya fedha hizo **Shilingi 538,121,000/=** ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 7,000,000,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

54. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, jumla ya **Shilingi 271,194,620/=** sawa na asilimia **4** ya makadirio zimepatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida na hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

55. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana pamoja na Baraza la Vijana Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ndogo hii ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi 538,121,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya **Shilingi 271,194,620/-** sawa na asilimia **50.3** zilipatikana. **Kiambatanisho 1D**

56. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi shughuli zifuatazo

zimepangwa kutekelezwa ambazo ni pamoja na kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Vijana nchini, kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, kusaidia na kuwawezesha Vijana kiuchumi na kuanzisha Kituo cha Vijana kitakachosaidia Vijana kupata huduma mbalimbali, kusaidia Mabaraza ya Vijana, kuhamasisha vijana kujiunga na Mabaraza ya Vijana na kushiriki katika shughuli za kizalendo.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya maendeleo ya Vijana nchini, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la UNFPA imefanikiwa kuendesha mikutano nane (8) ya Uratibu wa Maendeleo ya Vijana nchini (4 Unguja na 4 Pemba) ya kila robo mwaka kwa lengo la kutathmini na kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli za Maendeleo ya Vijana nchini kutoka kwa Taasisi na Wadau wa Maendeleo ya Vijana Zanzibar.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha umoja, Amani, upendo na maendeleo nchini, Wizara kwa Kushirikiana na Ofisi ya Waziri mkuu, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa kufanikisha kilele cha mbio za Mwenge 2021, Kumbukizi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na maadhimisho ya Wiki ya Vijana Kitaifa katika kijiji cha Chato Mkoani Geita.

Jumla ya Miradi **75** yenye thamani ya **Shilingi za Kitanzania 11,275,588,211.19/=** ilitembelewa na mengine kuzinduliwa. Uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa Mwaka 2022, umefanyika tarehe 2/04/2022 katika uwanja wa CCM sabasaba Mkoa wa Njombe na Mgeni Rasmi alikuwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ujumbe wa mwaka huu ni **"Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo, Shiriki Kuhesabiwa Tufikie Maendeleo ya Taifa''**.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Maendeleo ya Vijana imeendelea kufanya uhamasishaji na kuzitembelea shughuli za Kiuchumi za Vijana kwa lengo la kuwasaidia vijana kutatua changamoto zinazowakabili ikiwemo kuwaunganisha na fursa za mikopo na mafunzo. Jumla ya vikundi **128** vilitembelewa kwa mwaka 2021/2022 kati ya hivyo vikundi **30** Unguja na **98** Pemba. Vikundi hivyo vinajishughulisha na fursa za kilimo cha mboga mboga, ufugaji wa kuku, samaki na ufugaji wa nyuki katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba. Kufuatia ziara hiyo jumla ya vikundi na Taasisi **19** (**12** Unguja na **7** Pemba) wamepatiwa fedha taslim na vifaa vya kufanyia kazi kama vile vyarahani, computer, printer, Friza, mashine za boti, kama ufafanuzi zaidi unavyoonekana katika **kiambatanisho namba 2.**

60. **Mheshimiwa Spika,** kupitia maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya Vijana, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) imewapatia mafunzo vijana **460** (Unguja **300** na Pemba **160**) wakiwemo wanawake **183** na wanaume **277** juu ya shughuli za ufugaji samaki, majongoo ya pwani, kamba, ufugaji wa Nyuki, kuku, sungura na kilimo cha mboga mboga. Lengo la mafunzo hayo ni kupata taaluma ya vitendo ambavyo vitawasaidia Vijana kuanzisha na kufanya shughuli za kiuchumi zenye tija na kuongeza uzalishaji wao.

61. **Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza ushiriki wa Vijana wa kike katika shughuli za kiuchumi na uzalishaji, Idara ya Vijana kwa kushirikiana na Shirika la Youth Challenge International (YCI) kutoka Canada inatekeleza mradi wa miaka **5** wa "HerStart Innovative the Future" wenye lengo la kuwawezesha Vijana wa kike katika eneo la Ujasiriamali wa kijamii. Jumla ya vijana **746** wa Wilaya **5** za Unguja wamefikiwa. Aidha, Idara imekubaliana na Shirika hilo kuongeza Wilaya nyengine **6** zilizobaki katika utekelezaji wa mradi huo kuanzia mwezi Aprili, 2022.

62. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na UNICEF ilizindua Kampeni maalum ijulikanayo **"AMKA KIJANA"** iliyobeba ujumbe **"SHIRIKI KATIKA UCHUMI WA BULUU KWA**

**MAENDELEO ENDELEVU''**. Lengo la kampeni hii ni kushajiisha vijana kuanzisha shughuli za kiuchumi na kuwapatia taarifa juu ya fursa za uwezeshaji kiuchumi zilizopo kupitia fedha za uwezeshaji zilizotengwa na Serikali kupitia Programu ya kupunguza makali ya UVIKO 19. Jumla ya vijana **7,156** wakiwemo **2,916** kutoka Unguja na **4,240** kutoka Pemba na Vikundi **557** (Unguja **264** na Pemba **293**)vimefikiwa.

**63.** **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, kupitia Kampeni **Amka Kijana** Idara imefanikiwa kuongeza wanachama **2,000** wa Jukwaa la Kimtandao la Vijana (U-report) ambapo vijana hupata taarifa na kutoa maoni yao kwa njia ya simu juu ya maendeleo na ustawi wao wa kiafya na kiuchumi. Hadi sasa jukwaa hilo lina wanachama **13,000**. Vile vile, Wizara ilirusha Vipindi **2** na Documentary **1** kwa ajili ya Kampeni hiyo kupitia ZBC TV na Zanzibar Cable.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Maendeleo ya vijana kwa kushirikiana na UNFPA, UNICEF, FEED THE FUTURE pamoja na Taasisi mbali mbali za maendeleo ya vijana imetoa mafunzo ya uongozi, stadi za maisha na afya ya uzazi kwa vijana. Jumla ya vijana **500** wakiwemo **292** wanawake na wanaume **208** kutoka Wilaya zote walipatiwa mafunzo hayo. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imefanya mafunzo ya Utalii kwa Vijana

**20** wa kiume ili waweze kutumia fursa za Uchumi wa Buluu kupitia Utalii.

**65.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira ya kazi Idara imefanikiwa kununuwa kompyuta sita kwa ajili ya Maafisa vijana wa Wilaya Unguja na Pemba. Mfanyakazi mmoja amesaidiwa kupata mafunzo ya Muda mrefu ya Shahada ya Sanaa ya ustawi wa Jamii na mmoja amepatiwa mafunzo ya awali kazini (Induction course).

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Zanzibar **SUZA** limeweza kuwapatia Vijana **130** (wanawake **77** na wanaume **53**) mafunzo ya Uandishi wa Miradi pamoja na Mpango wa Biashara katika Wilaya zote za Unguja. Utekelezaji huu umeweza kuongeza uelewa wa Vijana juu ya uandishi wa Miradi pamoja na Mpango wa Biashara. Katika hatua nyengine, Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kati waliandaa mafunzo ya Utalii na uandishi wa miradi na Ujasiriamali ambapo jumla ya Vijana **90** wakiwemo wanaume **38** na wanawake **52** walipatiwa mafunzo hayo. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uelewa wa uandishi wa miradi na kutatua changamoto za ajira kwa Vijana.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na **"The Korea International Co-operation Agency"** (KOICA) limefanikiwa kufikia jumla ya vijana **24** (wanawake **10** na wanaume **14**) kuwapatia mafunzo ya uzalendo, mipango na uongozi huko Dar-es-Salaam kwa muda wa siku tisa (**9**). Matokeo baada ya mafunzo hayo ni kuweza kuongeza idadi ya Vijana wazalendo na kuipenda nchi yao. Sambamba na hilo, Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na **SOS** waliweza kutoa mafunzo ya Uongozi kwa Vijana **75** wakiwemo wanawake **40** na wanaume **35** wa Wilaya ya Magharibi "A'', Kaskazini "A" na Magharibi "B". Vijana **18** wa Baraza la Vijana kutoka Pemba waliweza kushiriki mashindano ya kombe la **"SHAMHUNA CUP"** kwa mchezo wa Pete.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kusaidia ofisi za Baraza la Vijana Wilaya **11** Unguja na Pemba kwa kuwapatia huduma za ofisi kama vile vifaa vya kuandikia, vifaa vya komputa, malipo ya maji, umeme na mafuta ili kuongeza ufanisi wa kazi. Vile vile, Baraza lilifanikiwa kuwapatia mafunzo ya awali kazini (induction caurse), maafisa sita (**6**), Unguja watano (**5**) na Pemba Mmoja. Vile vile Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kulipa stahiki za wafanyakazi **watatu** waliokwenda likizo.

69. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana limefanikiwa kuhamasisha vijana mbali mbali kujiunga na Baraza ambapo vijana wengi wamehamasika kujitokeza na kuchukuwa fomu katika Shehia zao na kufanya idadi ya wanachama wa Baraza la Vijana Zanzibar kuongezeka kutoka **18,833** na kufikia **21,094** wakiwemo wanaume **9,687** na wanawake **11,407** ni sawa na ongezeko la wanachama **2,261**.

70. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar liliandaa mafunzo maalumu kwa ajili ya Vijana na kuwafikia jumla ya Vijana **123** Unguja na Pemba, wakiwemo wanawake **61** na wanaume **62** waliomaliza Vyuo na Vyuo vikuu kwa kuwahamasisha na kuweza kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali na utoaji wa huduma lengo ni kuwapatia mafunzo na kuwaombea mikopo ili waweze kujiajiri. Vile vile, Baraza limefanikiwa kutoa taaluma ya matumizi sahihi ya sayansi na teknologia ya habari ambapo jumla ya Vijana **168** kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba wamefikiwa kwa ajili ya kupatiwa taaluma ya matumizi sahihi ya sayansi na teknolojia ya habari, Vijana **128** kwa upande wa unguja na Vijana **40** kwa upande wa Pemba.

71. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kufanya ziara ya kutembelea baadhi ya Miradi ya Baraza la Vijana kwa upande wa Pemba

jumla ya miradi nane (8) ya Vijana imetembelewa kwa lengo la kujua muendelezo na mafanikio ya miradi hio na kuimarisha shughuli za kiutendaji za Baraza pamoja na kuendeleza miradi ya Vijana. Miradi hiyo ni kilimo cha mbogamboga, uvuvi, ujasiriamali na ufugaji samaki. Vile vile, Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kuwapatia vijana **30** (wanaume **6** na wanawake **24)** mafunzo ya sanaa, uchoraji na uchongaji kwa muda wa miezi sita (**6**). Aidha, Baraza la Vijana Wilaya ya Micheweni limezinduwa darasa la kujifunza lugha za kigeni na utalii, jumla ya Vijana **90** (wanaume **50** na wanawake **40**) wameweza kujiunga na darasa hilo ili kufungua fursa za ajira kwa Vijana na kuweza kujiajiri wenyewe.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar lilifanikiwa kuwapatia elimu ya kuwajenga moyo vijana wa kuwa wazalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao ambapo jumla ya Vijana **205** walihudhuria katika mafunzo hayo. Vijana wameweza kushiriki katika shughuli za kuimarisha usafi, kushiriki katika ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kushiriki zoezi la upandaji wa mikoko katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Vile vile, Vijana **350** kutoka Pemba walishiriki katika kongamano la kuadhimisha siku ya Saba Saba. Hata hivyo, Baraza la Vijana Zanzibar liliendesha mafunzo ya siku tatu ya kuwajenga Vijana kuwa wazalendo kwa

Viongozi wa Baraza la Vijana ambapo jumla ya Vijana **112** (Unguja ni vijana **42** na Pemba **70**) walishiriki.

73. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar limeweza kufanya Kongamano la kuadhimisha miaka 58 ya Sherehe za Mapinduzi Zanzibar, ambapo jumla ya Vijana 150 waliweza kushiriki katika kong'amano hilo. Aidha, jumla ya Vijana 264 walishiriki katika kongamano la kuadhimisha matokeo tofauti ambayo ni siku ya UKIMWI duniani, uhamasishaji wa afya ya uzazi na jinsia pamoja na kumpongeza **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kutimiza mwaka mmoja wa Uongozi wake kupitia Wilaya tofauti. Pia, vijana **120** kutoka Baraza la Vijana Zanzibar wameweza kushiriki katika uzinduzi na matembezi ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora *''Foundation''* inayoongozwa na **Mama Maryam Mwinyi mke wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.**

**Mradi wa Maendeleo ya Vijana**

74. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maendeleo ya Vijana unatekelezwa ndani ya Programu ya Maendeleo ya Vijana. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umepangiwa kutumia **Shilingi 7,000,000,000/=** hadi kufikia Machi 2022, mradi huu haujaingiziwa fedha. Wizara

imefanikiwa kukamilisha taratibu za umiliki na upimaji wa maeneo ya Ujenzi wa Vituo vya Maendeleo ya Vijana Unguja na Pemba. Aidha, hatua za uandaaji wa Michoro na BOQ zinaendelea.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 imetengewa jumla ya **Shilingi 675,000,000/=** ambazo zimehaulishwa kutoka Mradi wa Maendeleo ya Vijana. Fedha hizo zimepangiwa kutekeleza mradi wa mashamba **2** ya kuku kwa Vijana (Pangeni Unguja na Mjini Ole Pemba) na Mradi wa Kiwanda cha ushoni kwa ajili ya mafunzo na kukuza ajira kwa Vijana (Limbani Pemba). Hadi kufikia Machi 2022, mradi haujaingiziwa fedha lakini Mkandarasi ameshapatikana na kukabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi.

**76.** **Mheshimiwa Spika,** sambamba na Miradi hiyo Wizara imedhamiria kuanzisha kiwanda cha ushoni cha vijana katika Mkoa wa Mjini Magharibi katika kijiji cha Bweleo Wilaya ya Magharibi B kupitia fedha za Mradi wa Pilipili. Hadi kufikia Machi 2022, Wizara imefanikiwa kununua banda litakalotumika kwa ajili ya mradi huo, jumla ya **Shilingi 112,0282,500/=** zimetumika sawa na asilimia **30** na Mkandarasi wa kulifanyia matengenezo banda hilo ameshapatikana.

### iii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 10,473,618,000/=** kati ya hizo, **Shilingi 3,473,618,000/=** ni matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 7,000,000,000/=** kwa ajili ya Mradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya **Shilingi 2,076,783,440/=** sawa na asilimia **20** zilipatikana. Kati ya hizo **Shilingi 1,955,783,444/=** ni matumizi ya kawaida, na **Shilingi 121,000,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Vile vile, Programu hii inaundwa na programu ndogo ya Maendeleo ya Utamaduni Sanaa na Michezo.

**Programu Ndogo: Maendeleo ya Utamaduni Sanaa na Michezo**.

78. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Maendeleo ya Utamaduni Sanaa na Michezo inatekelezwa na Idara ya Utamaduni na Sanaa, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, (BASSFU), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (COSOZA), Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 10,473,618,000/=** kati ya hizo, **Shilingi 3,473,618,000/=** ni matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 7,000,000,000/=** kwa ajili ya Mradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya **Shilingi 2,076,783,440/=** sawa na asilimia **20** zilipatikana. Kati ya hizo **Shilingi 1,955,783,444/=** ni matumizi ya kawaida, na **Shilingi 121,000,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. **(Tafadhali angalia Kiambatanisho Namba.1D).**

80. **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa ni uhifadhi, uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za Sanaa na wasanii, kurikodi kazi za Sanaa kupitia Studio ya Filamu na Muziki, uratibu wa kazi za Sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na Sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi fasaha ya Kiswahili, utoaji mafunzo kwa watendaji, wajasiriamali wa shughuli za kiutamaduni na wasanii pamoja na ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wenye hakimiliki.

81. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipanga kuimarisha na kuendeleza vituo vya michezo kwa ajili ya kuibua vipaji, kusaidia timu za Taifa, vilabu na Vyama vya Michezo kushiriki na kuandaa mashindano ya Kitaifa

na Kimataifa, kuandaa mashindano ya Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali. Aidha, Wizara ilipanga kusaidia viongozi wa vyama vya michezo, waamuzi na makocha kushiriki mafunzo ya Kitaifa na Kimataifa na kuimarisha uwanja wa Amaan, Gombani, Mao-Zedong na viwanja vya Wilaya.

82. **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza na kuendeleza utamaduni, Wizara imefanikiwa kuandaa Tamasha la 26 la Utamaduni wa Mzanzibari kwa Unguja na Pemba. Tamasha hili liliweza kuonesha sanaa mbali mbali za kiutamaduni, maonesho ya bidhaa na kazi za kiutamaduni, mavazi ya kiasili ya Kizanzibari, maonesho ya vyakula vya Kizanzibari na burudani kupitia ngoma za asili kutoka katika Wilaya za Unguja na Pemba pamoja na maonesho ya fensi.

83. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utamaduni imeendelea kurikodi vipindi vya redio kupitia ZBC kuhusu shughuli za Utamaduni na Sanaa kwa lengo la kuwahamasisha Wazanzibari hususan vijana kuendeleza Utamaduni wa Mzanzibari na kazi za sanaa. Kwa upande wa Studio ya Filamu na Muziki, Idara imefanikiwa kununua baadhi ya vipuri vya kompyuta inayotumika kurikodi sauti katika studio ya kuzalisha muziki (music production).

84. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanikiwa kufanya ziara ya kuwatembelea wajasiriamali wanaojishughulisha na sanaa ya ufinyanzi, ususi na uchongaji kwa lengo la kuona wanavyoendeleza shughuli zao na kusikiliza changamoto walizonazo. Jumla ya vikundi **6** vya wajasiriamali kutoka Wilaya ya Magharibi A na Magharibi B vilitembelewa na kupatiwa msaada. Sambamba na hilo, Idara kwa upande wa Pemba ilifanya ziara ya kutembelea vikundi vya wasanii na kuchagua kikundi kimoja kilichowakilisha kwenye Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika Januari 2022. Pia, Idara ya Utamaduni imefanikiwa kuwapatia mafunzo maafisa **5** wa Utamaduni Pemba yaliyohusu namna ya kuandaa matamasha ya kijamii.

85. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Kiswahili Zanzibar limefanikiwa kurusha hewani vipindi **50** vya Kiswahili lugha yetu kupitia ZBC TV na Redio, Zenji FM, Star TV, AZAM TV, ZCTV, TBC TV na Redio, Habari FM Redio, Redio One, UFM Redio, Redio ya Ujerumani na Redio UN. Kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Aidha Maneno **76** ya vipeperushi vya msamiati (Kamusini Leo) yamerushwa katika mitandao ya kijamii.

86. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Kiswahili Zanzibar limeshiriki katika Kongamano la Idhaa za Kiswahili

duniani lililofanyika mwezi machi 2022, Arusha. Katika kongamano hilo jumla ya Makala **10** ziliwasilishwa zikiwemo za Taaluma ya Kiswahili na za Afya. Aidha, Tunzo za Heshima kwa kukuza na kuendeleza Kiswahili zilitolewa kwa **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanikiwa kuandaa kongamano la Tano la Kiswahili la Kimataifa lililofanyika Zanzibar mwezi Oktoba 2021, lililojumuisha maonesho ya vitabu na uwasilishaji wa makala elekezi kuhusu maendeleo ya Kiswahili na TEHEMA. Jumla ya washiriki **298** kutoka Tanzania Bara, Kenya na wenyeji wa Zanzibar walishiriki.

**88.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kutangaza machapisho ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar ambapo jumla ya machapisho **27** yameuzwa yakiwemo Kamusi la Kiswahili Fasaha, Kamusi la lahaja ya Kitumbatu, Kamusi la lahaja ya Kipemba, Kamusi la lahaja ya Kimakunduchi, Jarida la Jahazi, Kitabu cha Mawasiliano ya Msingi ya Kiswahili kwa Wageni na Kitabu cha Utamaduni wa Mzanzibari. Kwa mwaka 2022/23, Baraza la Kiswahili Zanzibar limejipanga kutangaza machapisho yake kupitia

mitandao ya kijamii, Mikutano ya kitaaluma na kwenye Maonyesho.

89. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) katika kuhakikisha inasimamia maadili ya kizanzibari yasipotee na kuwa na Sanaa yenye kuonesha maadili yalio mema pamoja na udhibiti wa kazi za sanaa, imefanikiwa kukagua kazi za sanaa za monesho **177**. Kazi hizo zimefanyiwa ukaguzi kwa kuzifanyia uhakiki wa kutolewa makosa ya kisanaa na maelekezo ya maadili ili ziweze kutumika hadharani. Aidha vikundi **131** vya Sanaa na Utamaduni vimesajiliwa upya kwa ajili ya kufanya kazi zake kwa mujibu ya sheria ya BASSFU namba **7** ya mwaka 2015. Pia, Baraza la Sanaa,Sensa ya Filamu na Utamaduni limefanikiwa kurusha hewani jumla ya vipindi **36** vya Redio na Televisheni

90. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza la Sanaa Sensa ya Filamu na Utamaduni inavitahadharisha vikundi vyote vya Sanaa na wasanii kuheshimu Utamaduni wa Mzanzibari kwa kufuata kanuni na sheria zilizowekwa. Wizara haitosita kuvichukulia hatua vikundi vitakavyokwenda kinyume na kuchafua Mila, Silka na Utamaduni wetu. Baraza limewasaidia wasanii wa Zanzibar kushiriki katika mashindano ya Tanzania na msanii mmoja amepata tuzo. Pia, kikundi cha taarab cha Rahatul Zaman kilishiriki

katika maoyesho ya biashara ya Dubai, Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia alikuwepo kwenye maonyesho hayo na kuburudika na wananchi wengine.

91. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kusimamia na kulinda haki na maslahi ya wasanii na wabunifu wa kazi za sanaa jumla ya kazi **514** za hakimiliki zimesajiliwa na kuingizwa katika mfumo wa Usajili. Kazi hizo ni Muziki wa Kizazi Kipya **131**, Kasida **58**, Nyimbo za Injili **87**, Filamu **75**, Taarab **1**, Mashairi **2**, Mawaidha "Volume" **26**, Makala **3**, Vitabu **20**, Maandishi ya Miradi **18** na Picha za michoro **3**. Idadi ya usajili wa kazi za sanaa inaongezeka kutokana na wasanii na wabunifu kuwa na imani ya usimamizi mzuri wa kazi zao unaofanywa na Afisi ya Hakimiliki Zanzibar.

92. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukusanyaji wa mirabaha, Afisi imefanikiwa kukusanya **Shilingi 100,487,394/=** ambazo zitagaiwa kwa wasanii na wabunifu **1500** wa vikundi mbali mbali vya sanaa na ubunifu Unguja na Pemba ifikapo Juni 30, 2022. Wanufaika wa mgao huo ni wale ambao wamesajili kazi zao katika Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar. Aidha, athari za janga la Uviko 19 bado ni changamoto kwa wadau wetu kulipia mirabaha.

93. **Mheshimiwa Spika,** katika kupunguza uharamia wa hakimiliki, Afisi imefanya ukaguzi wa maeneo ya

watumiaji **332** kwa lengo la kuhakikisha matumizi halali ya kazi za sanaa na ubunifu. Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni Hoteli **129**, “Video Library” **105**, Viwanja vya kufurahishia watoto **3**, Kumbi za burudani **19**, Taasisi za elimu **6** na Maduka ya kutoa fotokopi **58**. Ukaguzi umebaini kuwapo kwa kiasi kikubwa cha uharamia hasa katika “wauzaji wa vinasa sauti na picha za kielektoniki”. Hata hivyo, wameendelea kuelimishwa juu ya kufata taratibu na Sheria.

94. **Mheshimiwa Spika,** jukumu la kutoa elimu juu ya masuala ya hakimiliki ni endelevu, lengo ni kuifanya Zanzibar kuwa ni sehemu yenye kuheshimu masuala ya Hakimiliki. Hivyo, Afisi imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanafunzi kuwa na utamaduni wa kuheshimu kazi za maandishi wanazozitumia ikiwa ni pamoja na kufuata utaratibu wa kunukuu na kutaja chanzo husika cha kazi hiyo. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wanafunzi **30** wa skuli ya Sekondari Madungu. Aidha, Afisi imerusha hewani vipindi **6** kupitia ZBC TV, Redio Jamii ya Micheweni na Mkoani kwa ajili ya kuwaelimisha wasanii juu ya umuhimu wa kusajili kazi zao.

95. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Hakimiliki imewafikia wasanii **10** wagonjwa katika maeneo yao na wamepatiwa kiasi cha fedha cha **Shilingi 100,000/=** kwa kila mmoja, kinachotokana na eneo maalum la

mirabaha. (Unguja **5** na Pemba **5**). Pia, Afisi imewapatia msaada wa vifaa vya uchoraji na Kompyuta moja kwa Chama cha Wasanii Wachoraji Zanzibar kwa ajili ya kukuza kiwango cha shughuli zao cha Uchoraji.

**96.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutatua migogoro ya hakimiliki, Afisi imepokea Malalamiko **7** ya uvunjwaji wa hakimiliki. Malalamiko **5** yameshapatiwa ufumbuzi na **2** yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi. Naomba nichukue fursa hii kuiomba jamii ya Wazanzibari kuacha kutumia kazi za hakimiliki kinyume na utaratibu unaofaa.

**97.** **Mheshimiwa Spika,** mfano wa makosa yanayofanywa ndani ya jamii yetu na kuonekana ni jambo la kawaida ni kile kitendo cha nyimbo za kikundi kimoja kuimbwa na kikundi chengine bila ya ridhaa ya kikundi husika; kutoa nakala (copy) nyingi za vitabu vya waandishi wa ndani au nje ya nchi bila ya ridhaa ya wamiliki wenyewe; wanafunzi kunakili kazi zilizoandikwa na wengine na kuzifanya zakwao bila ya kumtaja mtunzi wa kazi hizo. Kufanya hivyo ni makosa kwa mujibu wa Sheria. Halikadhalika, kufanya hivyo ni kuwakosesha haki zao wasanii na wabunifu waliojiajiri katika tasnia hii ya sanaa na ubunifu.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza michezo nchini, Idara ya Michezo imeruhusu uwanja wa Amaan kutumika kama uwanja wa nyumbani kwa mechi

ya Klabu bingwa ya Afrika na pia mechi ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Aidha, Idara ya Michezo iliisaidia timu ya KMKM kusafiri na kushiriki mechi za mashindano ya klabu Bingwa Afrika yaliyofanyika Tunisia mwezi wa Septemba, 2021 na kuisaidia timu ya Mafunzo kusafiri na kushiriki mechi za mashindano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika yaliyofanyika Angola mwezi Septemba, 2021. Pia, Shirikisho la Mpira wa Miguu la Viziwi (SHIMIVIZA) lilisaidiwa kushiriki mashindano ya kimataifa ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu wa uziwi yaliyofanyika nchini Kenya.

99. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Michezo ilikisaidia Chama cha Netball Zanzibar (CHANEZA) kulipia ada ya uanachama na ada ya mashindano ya Kombe la Netboli la Afrika ambayo yalifanyika Namibia mwezi Novemba 2021. Aidha, Idara imefanikiwa kuliombea uwanachama wa kudumu Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu wa mguu mmoja na mkono mmoja Zanzibar (ZAFF) katika Shirikisho la mchezo huo barani Afrika (CANAF). CANAF ni miongoni mwa mashirikisho machache ambayo yamekubali kuisajili Zanzibar kuwa mwanachama wa kudumu. Vile vile, Shirikisho la ZAFF limelipiwa ada ya uanachama na ada ya mashindano ambapo mwezi Oktoba 2022, Timu ya Taifa ya Zanzibar ilishiriki mashindano ya Kimataifa ya Afrika yaliyofanyika Dar es Salaam.

100. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Michezo ilifanikiwa kuendesha mashindano ya mchezo wa Baskeli na mashindano ya Ngalawa yaliyofanyika Tumbe kiswani Pemba mwezi Agosti 2021. Mashindano hayo yanalenga kuifufua na kuiendeleza michezo hiyo ya asili ambayo imeanza kutoweka hapa Zanzibar. Aidha, Chama cha Mchezo wa Mpira wa Kikapu Zanzibar (BAZA) kiliwezeshwa kufanya fainali za ligi ya Zanzibar ya mchezo huo ambayo ilifanyika mwezi Novemba mwaka 2021 kisiwani Pemba.

101. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Michezo kwa kushirikiana na taasisi ya Coaches Accross Continents (CAC) imefanikiwa kuratibu mafunzo ya utumiaji wa michezo katika kutatua changamoto zilizopo katika jamii (Purposeful Play) kwa walimu na viongozi wa michezo mbali mbali. Jumla ya washiriki **125** wamepatiwa mafunzo hayo Unguja **50** na Pemba **50**. Sambamba na hilo, wanamichezo wanawake **25** kutoka Unguja wamepatiwa mafunzo maalum ya uongozi kwenye michezo (women leaders programme) ambayo yaliendeshwa na wakufunzi kutoka Uingereza, Canada na Marekani.

102. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Michezo iliandaa mashindano mbali mbali ikiwemo mpira wa miguu, kuvuta kamba na mchezo wa nage kwa timu za Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali.

Mashindano hayo yaliweza kusaidia kuleta hamasa ya michezo na mazoezi kwa watumishi wa umma ambapo jumla ya timu **24** za mpira wa miguu kutoka Wizara na Mashirika ya Serikali zilishiriki.

**103.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Michezo imefanikisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yalifikia kilele chake tarehe **13** mwezi Januari 2022, katika uwanja wa Amaan Zanzibar. Jumla ya timu **10** zilishiriki katika mashindano hayo zikiwemo sita kutoka Zanzibar na nne kutoka Tanzania Bara. Timu zilizoshiriki kwa upande wa Zanzibar ni timu ya Mlandege, Taifa Jangombe, KMKM, Meli Nne City, Yoso Boy na Selem View na kwa upande wa Tanzania bara ni timu ya Simba SC, Young African, Azam FC na Namungo FC. Vinara wa mashindano hayo kwa mwaka 2022 ni Simba Sports Club ya Dar es Salaam.

**104.** **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuhamasisha mazoezi ya viungo hapa Zanzibar kwa lengo la kujenga afya, kuleta upendo na umoja baina ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla, Wizara imefanikisha kuadhimisha siku ya Mazoezi ya viungo kitaifa yaliyofanyika mwezi wa Januari, 2022. Mgeni rasmi katika siku hii alikuwa **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.** Zaidi ya wananchi **4,500** walishiriki

tamasha hilo na vilabu vya mazoezi **130** vikiwemo **90** kutoka Unguja, **19** kutoka Pemba na **21** kutoka Tanzania Bara vilishiriki.

**105.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar Idara ya Michezo imefanya maboresho makubwa katika uwanja wa Amaan kwa kuweka taa za minara, kukarabati vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji, ununuzi wa samani katika Ukumbi wa VIP, ununuzi wa vitanda kwa ajili ya ukaguzi wa wachezaji, ukarabati wa paa katika eneo la VIP, kutia rangi, usafishaji wa nguzo za eneo la VIP, kufanya matengenezo ya vipoza hewa na matengenezo ya mfumo wa sauti (PA System).

**106.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na utaratibu wa kukuza na kuendeleza vipaji vya waamuzi wadogo kwa mpira wa miguu. Ambapo jumla ya vijana **21** wanapatiwa mafunzo hayo katika kituo cha michezo cha JKU (JKU sports Academy) kilichopo Kama. Ni matumaini yetu kuwa vijana hawa watakuwa waamuzi bora katika kutekeleza wajibu wao na kuziba pengo la uchache wa waamuzi wenye sifa hapa Zanzibar. Waamuzi hawa ndio waliotumika kuchezesha mashindano ya Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali yaliyofanyika mwezi Disemba na kufikia kilele mwezi Januari 2022.

107. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar limefanikiwa kuvisaidia vyama **10** vya michezo kushiriki na kuandaa mashindano ya ndani na kitaifa. Vyama vilivyosaidiwa ni Chama cha Judo, Squash, Basketball, Volleyball, Baseball na Softball, Netball, Shotokan, Handball, Riadha, Mpira wa meza pamoja na Kuogelea. Kwa upande wa mchezo wa Baseball na Softball timu za Zanzibar zilifanya vizuri kwenye mashindano ya kitaifa yaliyofanyika Dar es Salaam. Adha, timu hizo zilipata nafasi ya kwanza na ya pili na kuzawadiwa vikombe, medali za dhahabu **12** na medali za fedha **12**. Pia, wachezaji **7** kutoka Zanzibar wamechaguliwa kushiriki mashindano ya kimataifa yatakayofanyika Japan mwezi wa Juni, 2022.

108. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar limefanikiwa kutoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi pamoja na utafutaji masoko katika michezo kwa viongozi wa vyama vya michezo. Jumla ya viongozi **50** wa vyama vya michezo wamepatiwa mafunzo hayo.

109. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limevisaidia vyama vitatu (3) vya michezo ya watu wenye ulemavu katika kuandaa na kushiriki mashindano mbali mbali yakiwemo mashindano ya Taifa ya michezo ya watu wenye ulemavu wa akili yaliyofanyika

Mwanza ambapo Zanzibar ilifanikiwa kupata medali **20** zikiwemo dhahabu **8**, fedha **1** na shaba **11** katika michezo tofauti. Wizara inawapongeza sana vijana wetu wenye ulemavu wa akili kwa ushindi walioupata. Vyama vyengine vilivyosaidiwa ni Shirikisho la Michezo ya Viziwi pamoja na Chama cha michezo ya watu wenye ulemavu wa viungo.

110. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanikisha kufanya marekebisho ya katiba ya Chama cha Basketball na Shirikisho la Michezo ya Viziwi pamoja na kufanikisha uchaguzi wa viongozi wa Shirikisho hilo.

111. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar inaendelea kuinuka kimichezo ambapo timu zetu za vijana wamekuwa wakiibuka kidedea kwa kuchukuwa vikombe vya mashindano mbali mbali ikiwemo kwenye mashindano ya Mama Samia Cup kwa mchezo wa mpira wa miguu Mkoa wa Mjini Magharibi umeibuka mshindi, Mchezo wa riadha Mkoa wa Kusini Unguja umefanikiwa kuchukuwa kikombe na kwa mashindano ya mpira wa miguu UMISETA Pemba ilifanikiwa kuchukuwa kombe.

**Mradi wa uimarishaji wa Viwanja vya Michezo**

112. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa uimarishaji wa Viwanja vya Michezo unatekelezwa ndani ya

programu ndogo ya uimarishaji na uendelezaji wa Michezo ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ulidhinishiwa kutumia **Shilingi 4,000,000,000/=**. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya **Shilingi 121,000,000/=** sawa na asilimia **3** zimepatikana.

**Mradi wa Ujenzi wa Viwanja Vya Michezo na Akademia**

113. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa ndani ya programu ndogo ya uimarishaji na uendelezaji wa Michezo, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 uliidhinishwa kutumia **Shilingi 3,000,000,000/=**. Hadi kufikia Machi 2022, Mradi huu haujaingiziwa fedha.

**iv Programu ya Uendelezaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo**

114. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii iliidhinishiwa **Shilingi 2,761,735,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2022, jumla ya **Shilingi 1,717,134,870/=** sawa na asilimia **62** zilipatikana. Programu hii inaundwa na programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara na Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia shughuli za Wizara Pemba.

**Programu ndogo 1: Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**

115. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,683,025,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2022 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,060,048,000/=** sawa na asilimia **63**. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D)**.

116. **Mheshimiwa Spika,** shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi vifaa vya ofisi na vitendea kazi; kuwajengea uwezo wafanyakazi na kulipa stahiki zao na kuandaa mpango wa manunuzi na mpango wa matumizi ya fedha.

117. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuimarisha maeneo ya ofisi ya Wizara ikiwemo sehemu za masjala, eneo la ukumbi wa Wizara, kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi na vifaa mbalimbali vya kazi. Aidha, Wizara imewapatia likizo wafanyakazi **289** na kulipwa stahiki zao. Vile vile, Wizara imeandaa database ya taarifa zote muhimu za wafanyakazi na

kusimamia utekelezaji wa mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano.

118. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kutoa mafunzo ya ndani kwa Wakuu wa Taasisi za Wizara ya Habari, Wahasibu, Keshia na Maafisa manunuzi wa Wizara juu ya kanuni na sheria za manunuzi. Mafunzo haya yalilenga kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu ya kila siku ndani ya wizara. Aidha, wafanyakazi **37** ikiwemo **16** wanawake na **21** wanaume wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi katika ngazi na taaluma tofauti. Sambamba na hilo wafanyakazi **67** wamepatiwa mafunzo ya awali kazini (*induction course*) na kuombewa kuthibitishwa kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014. Wizara imeendelea kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji wake kulingana na taaluma na nafasi zao za kazi kupitia Idara na Taasisi zake.

119. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kufanya mikutano miwili (2) ya wafanyakazi ikiwemo mmoja (1) Unguja na mmoja (1) Pemba juu ya kuwaelekeza wafanyakazi kuhusu utekelezaji wa majukumu yao na kubadilishana mawazo ya kiutendaji jambo ambalo hufurahiwa sana na wafanyakazi. Idara imeratibu Mikutano ya Kamati ya Uongozi na Kamati Tendaji ya

Wizara kwa lengo la kuongeza ufanisi na kasi kubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

120. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa sherehe na hafla mbalimbali zinazoratibiwa na Wizara ikiwemo hafla ya uchangishaji fedha kwa ajili ya Maendeleo ya Michezo Zanzibar iliyofanyika katika Hoteli ya Madinat Al Bahr katika hafla hii jumla ya Shilingi Milioni mia tisa na arubaini (**940,000,000/=**) ziliahidiwa na wadau mbali mbali. Pia, Wizara iliandaa sherehe ya kumpongeza **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** iliyofanyika katika Hoteli ya Sea Cliff Mkoa wa kaskazini Unguja. Aidha, Idara imesimamia ziara za kikazi kwa viongozi wakuu wa Wizara kwa upande wa Pemba na Tanzania Bara. Ziara hizo zimeweza kuimarisha ushirikiano na wadau wa Wizara pamoja na kusimamia kwa ukaribu utendaji wa kazi katika Taasisi zilizomo chini ya Wizara.

121. **Mheshimiwa Spika,** katika kuleta ufanisi mzuri wa matumizi ya rasilimali fedha, Idara imefanikiwa kufanya ukaguzi wa ndani na kutoa ripoti za fedha kwa kila robo mwaka kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma yanafanyika kwa usahihi. Wizara pia imesimamia nidhamu kazini kwa kutembelea taasisi zake mbali mbali Unguja

na Pemba na kuwaonya wafanyakazi wanaokiuka kanuni za Utumishi wa Umma.

**Programu Ndogo 2: Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

122. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka 2021/2022 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 155,600,000/=** na hadi kufikia Machi 2022 imefanikiwa kupata jumla ya **Shilingi 44,000,000/=** sawa na asilimia **28**. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D)**.

123. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa, kuandaa mipango na kutayarisha bajeti ya Wizara, kuratibu na kusimamia Sera za Wizara, kufanya tafiti za Wizara, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi na programu za Wizara, kuandaa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuziwasilisha, kuratibu vikao na ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na Kuratibu na Kusimamia vikao vya Ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

124. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa taarifa za utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ikiwemo taarifa za utekelezaji wa bajeti, taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025 pamoja na taarifa za ufuatiliaji na tathmini za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Idara imeandaa mpango wa matumizi wa muda wa kati (MTEF), Mpango wa utekelezaji wa mwaka mmoja pamoja na hotuba ya bajeti kwa mwaka 2022/2023.

125. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanya ufuatiliaji na tathmini juu ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa upande wa Unguja na Pemba. Miradi iliotembelewa ni Miradi ya Vijana ya Green house na visima, viwanja vya michezo vya Wilaya na maeneo yaliyofanyiwa upimaji kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vidogo vidogo (4 in 1) Pemba, eneo litakalojengwa Bwawa la kuogelea la kisasa lililopo Amaan na eneo la ujenzi wa akademia ya Michezo lililopo Mwehe Makunduchi.

126. **Mheshimiwa Spika,** Kufuatia masuali mbali mbali ya waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi, Wizara imefanya utafiti mdogo juu ya uwanzishwaji wa Michezo ya ngumi hapa Zanzibar. lengo la utafiti huo ni kupata maoni ya wananchi kuhusiana na kuanzishwa kwa michezo ya ngumi kuchezwa Zanzibar, utafiti uliwashirikisha wananchi wapatao **5,702** na kati ya hao wananchi **3614** sawa na

asilimia **63** waliohojiwa walisema kuwa michezo hiyo iruhusiwe ambapo wananchi **2,088** sawa na asilimia **37** walikuwa na mtazamo tofauti. Hali hii inaonesha kwamba wazanzibari walio wengi wanapendelea michezo hii iruhusiwe kuchezwa hapa visiwani.

**127.** **Mheshimiwa Spika,** Idara imeweza kuratibu vikao **3** vya ushirikiano na Wizara zenye dhamana ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo za SMT na SMZ vilivyofanyika Dodoma na Zanzibar. Wizara imefanikiwa kujadili na kutatua baadhi ya changamoto zilizokuwepo. Kwa mfano, kushirikiana baina ya BAKIZA na BAKITA katika shughuli za uundaji wa Istilahi na ukuzaji wa Kiswahili, kuonekana kwa ZBC kama free chanel kupitia ving'amuzi vya AZAM Media, Star Times, DSTV, ZCTV na Coconut.

**128.** **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanikiwa kuratibu vikao na ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi ikiwa ni muendelezo wa usimamizi mzuri wa shughuli za Serikali. Tunawashukuru sana Wenyeviti na wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Kamati ya Bajeti, Kamati ya PAC na Kamati ya LAAC kwa namna tunavyoshirikiana na mnavyotupa miongozo na maelekezo ambayo husaidia sana katika utekelezaji wa shughuli zetu za Wizara ya Habari.

129. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango kwa kushirikiana na maafisa kutoka Tume ya Mipango Zanzibar inakamilisha Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa miaka mitano utakao toa muelekeo katika utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa kipindi kinachoanzia mwaka 2022/23 hadi 2026/27. Vile vile, Wizara kupitia Idara ya Mipango imewasilisha Serikalini nyaraka tatu kwa ajili ya kutolewa maamuzi. Nyaraka hizo ni kuhusu Uanzishwaji wa Michezo ya Ngumi hapa Zanzibar, Usimamizi wa Maafisa Habari na Mawasiliano wa Taasisi za Serikali na Uimarishaji wa Kampuni ya Serikali ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui (ZMUX). Nyaraka zote tatu zimeshatolewa maamuzi.

130. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Idara imekamilisha hatua za mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2005, Sera ya Habari ya mwaka 2006 na Sera ya Utamaduni ya mwaka 2005 hatua inayosubiriwa ni kuwasilishwa katika vikao vya Makatibu Wakuu baada ya kukamilika muongozo wa uandaji wa sera za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Idara inaendelea na hatua za ukamilishaji wa sera ya Lugha ya Kiswahili ya mwaka 2022 na Sera ya Filamu ambazo ipo katika hatua za vikao vya Wizara, sambamba na kufanya marekebisho sheria ya habari na sheria ya hakimili.

**Programu ndogo 3: Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba**

131. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba ambayo ina jukumu la kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 923,110,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2022, imefanikiwa kupata jumla ya **Shilingi 613,086,020/=** sawa na asilimia **66**. **(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1D)**.

132. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa kuratibu shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba ikiwemo kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi wa Ofisi kuu Pemba, kutoa uelewa kwa wafanyakazi kuhusiana na masuala mbalimbali katika kuimarisha utendaji kazi, kusimamia shughuli za miradi inayotekelezwa Pemba na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiutendaji za Wizara zinazofanyika Unguja na nje ya Zanzibar.

133. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi huduma

ya vitendea kazi na vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kiutendaji. Sambamba na hilo, wafanyakazi wamepatiwa stahiki zao kama vile malipo baada ya saa za kazi, fedha za likizo, haki ya likizo la kawaida na likizo la uzazi kwa mama na baba baada ya kujifungua mtoto. Aidha, ofisi inaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba na kusimamia utekelezaji wa mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano.

**134. Mheshimiwa Spika,** Mfanyakazi mmoja amepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya stashahada na wafanyakazi **5** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ikiwemo mafunzo ya awali kazini (*induction course*). Sambamba na hayo, wafanyakazi **11** wameombewa kuthibitishwa kuwepo kazini baada ya kutimiza vigezo na masharti kama ilivyoelezwa kwenye kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

**135. Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanikiwa kuratibu ziara za viongozi katika Wilaya zote za Pemba. Shughuli zilizotembelewa ni pamoja na vikundi vya wajasiriamali vijana, vikundi vya sanaa, shughuli za utamaduni na vyama vya michezo kwa lengo la kuwahamasisha na kutatua migogoro iliyojitokeza. Aidha, Ofisi imeendelea kuratibu ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi za kutembelea miradi ya

Wizara kwa upande wa Pemba. Vile vile, shughuli ya kukusanya takwimu za vikundi vinavyojishughulisha na kazi za Utamaduni na Sanaa imefanywa katika Wilaya ya Micheweni. Jumla ya vikundi **36** vikiwemo **12** vya dufu, **16** Sanaa za Maigizo na na **8** Sanaa nyengine za kiutamaduni vimerikodiwa taarifa zake.

**136.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara, Ofisi kuu Pemba imefanya ufuatiliaji na tathmini wa Miradi na shughuli zinazotekelezwa kwa upande wa Pemba. Miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji ni pamoja na miradi ya kiuchumi ya vijana, vikundi vinavyojishughulisha na kazi za sanaa na viwanja vya Michezo vikiwemo vya Wilaya. Ziara hizi zimesaidia kutatua changamoto mbali mbali na kuongeza ushirikiano kwa wadau wa Wizara. Pia, Ofisi ilifanya ziara ya kuwatembelea vijana **160** waliopatiwa mafunzo ya vitendo kuhusu kilimo cha mboga mboga, ufugaji wa samaki, ufugaji wa nyuki na ufugaji wa sungura. Mafunzo hayo yamewasaidia sana na kuwajenga ari ya kuanzisha mashamba yao ya kilimo na ufugaji.

**137.** **Mheshimiwa Spika,** taarifa za utekelezaji wa bajeti na taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa wakati. Aidha, Ofisi Kuu Pemba imetayarisha hotuba ya bajeti, Mpango wa Matumizi wa Muda wa

Kati (MTEF) na Mpango Kazi na kuziwasilisha Ofisi Kuu Unguja.

## E. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**138.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imetengewa jumla ya **Shilingi 49,081,861,000/=**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 16,344,600,000/=** sawa na asilimia **33** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 32,737,261,000/=** sawa na asilimia **67** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**139.** **Mheshimiwa Spika,** kwa matumizi ya kazi za kawaida jumla ya **Shilingi 8,385,000,000/=** ni kwa ajili ya mishahara ambapo **Shilingi 4,024,100,000/=** ni mishahara ya Idara za ndani ya Wizara na **Shilingi 4,360,900,000/=** ni mishahara kwa taasisi zinazopokea ruzuku.

**140.** **Mheshimiwa Spika,** kwenye matumizi mengineyo, jumla ya **Shilingi 8,029,600,000/=** kati ya hizo **Shilingi 2,940,800,000/=** ni matumizi mengineyo kwa Idara za Wizara na **Shilingi 5,018,800,000/=** kwa taasisi zinazopokea ruzuku. Kwa fedha za miradi ya maendeleo, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi**

**32,737,261,000/=** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. **(Tafadhali angalia kiambatanisho 1F na 1G)**

141. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 9,487,897,000/=** kati ya hizo **Shilingi 875,997,000/=** ni mapato yanayoingia hazina na **Shilingi 8,611,900,000/=** ni mapato yanayotumiwa na Taasisi husika. **(Tafadhali angalia kiambatanisho 1H na 1J)**

## F. MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

142. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imejipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo :-

i. Kuimarisha Miundombinu ya Habari kwa ajili ya uzalishaji na urushwaji wa vipindi bora, ununuzi wa mitambo ya kisasa ya kurushia matangazo; ununuzi wa maudhui, ufuatiliaji wa habari na kuboresha huduma za Bohari na Uchapaji;

ii. Kuongeza nakala za Magazeti kutoka 1,482,000 hadi 1,485,500 kwa mwaka, kuongeza maeneo ya usambazaji magazeti kutoka Mikoa 11 hadi 16 Tanzania Bara; kuongeza Mawakala kutoka

10 hadi 18; kuimarisha huduma za kimtandao na kuimarisha miundombinu ya Shirika na vitendea kazi;

iii. Kuhamasisha vijana wachangamkie fursa za ajira, kuwajengea uwezo, kuimarisha huduma za Vijana kwa kuanzisha Vituo viwili vya Maendeleo ya Vijana Unguja na Pemba na Kuratibu mbio za mwenge wa Uhuru kitaifa;

iv. Kuimarisha huduma za utamaduni na sanaa kwa kujenga Nyumba ya Sanaa kwa lengo la kutoa mafunzo, kuongeza ajira, kukuza, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, Sanaa na ubunifu kwa jamii ya Zanzibar ili haki na maslahi ya wasanii na wabunifu zipatikane;

v. Kuendeleza, kukuza na kueneza Kiswahili kuwa kama bidhaa kwa kuandaa mpango wa Kiswahili na kufuatilia fursa zilizopo za mahitaji ya Kiswahili ndani na nje ya nchi;

vi. Kuratibu maendeleo ya michezo na kuimarisha miundombinu ya michezo pamoja na kuviwezesha vyama vya michezo kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa Sera, Sheria ya Baraza na kanuni za mashirikisho ya michezo ya kimataifa, kikanda na Kitaifa na kuzisadia timu za Taifa na za watu wenye ulemavu Kushiriki kwenye mashindano na kushiriki katika bonanza la kitaifa la Mazoezi;

vii. Kukamilisha Sera, Sheria na Kanuni za Wizara

ambazo zimefanyiwa mapitio ili ziweze kutumika na kufanya Tafiti katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; na

viii. Kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi na wafanyakazi ikiwemo utoaji wa vitendea kazi na stahiki za wafanyakazi kwa mujibu wa sheria na kuwaendeleza kwa kuwapatia mafunzo.

## G. PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**143. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, itaendelea kutekeleza Programu Kuu 4 na Programu ndogo 8 chini ya Fungu J03 kama ifuatavyo:-

**Programu Kuu PJ0301: Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji (Tshs 22,980,061,000/=)**

**144. Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongezeka kwa upatikanaji na usambazaji wa habari za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi kwa wananchi kwa wakati. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwa wananchi wanapata huduma na kutumia habari zenye kiwango bora kwa maslahi yao na taifa. Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari; na
ii. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji.

**145. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kuboresha huduma ya utoaji wa taarifa, picha, makala, filamu na sinema kuwa ya kisasa ili kuwafikia wananchi wote wa Zanzibar;
2. Kuzalisha na kurusha vipindi na matangazo kupitia ZBC TV na Redio;
3. Kusambaza maudhui ya utangazaji kupitia Kampuni ya ZMUX na kuongeza chanali pendwa kwa watazamaji;
4. Kuchapisha Gazeti la kila siku la Zanzibar Leo, Magazeti ya kila wiki Zanzibar Mail, Zanzibar Leo Jumapili, ZaSpoti na Gazeti la kila mwezi Zanzibar Leo Wanawake na kuyasambaza;
5. Kudhibiti na kusimamia shughuli za Utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji;
6. Kuboresha huduma za bohari kwa kuongeza vifaa vya ofisi na kuandikia na kununua mitambo ya kisasa ya uchapaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa kazi za uchapaji;

7. Kudhibiti na kusimamia shughuli za vituo vya utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji;
8. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Mashirika na kampuni zilizomo ndani ya Wizara kwa kuwapatia mafunzo ili kuendana na kasi ya Teknolojia inayokuwa kwa haraka duniani na kuleta ufanisi katika kazi zao; na
9. Kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanya kazi kwa kuwapatia vifaa vya kisasa na kulipa stahiki zao.

**146. Mheshimiwa Spika,** ili programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 22,980,061,000/=**. Kati ya hizo **Shilingi 8,642,800,000/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 14,337,261,000/=** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Programu Kuu PJ0302: Maendeleo ya Vijana (Tshs 7,045,799,000/=)**

**147. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii, ni kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha vijana waweze kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia programu mbali

mbali. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuongeza idadi ya ajira kwa vijana kwa kuwajengea uwezo na kuwaunganisha na fursa za ajira zilizopo. Programu hii itakuwa na Programu ndogo moja sambamba na Mradi wa Maendeleo ya Vijana.

148. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kuwajengea uwezo vijana kwa kuwapatia mafunzo kwenye shughuli za ujasiriamali, elimu ya stadi za maisha na afya ya uzazi; kuwaunganisha na taasisi za mikopo nafuu, kuwasaidia kutafuta masoko na fursa za ajira;
2. Kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru Kitaifa pamoja na kuwapatia vijana elimu ya uzalendo kwa lengo la kuipenda nchi yao;
3. Kuyawezesha Mabaraza ya Vijana ya Wilaya kwa kuyapatia mafunzo ya uongozi, kuwa na ofisi, samani za ofisi, wafanyakazi pamoja na kuwaunganisha vijana katika fursa mbalimbali za kijamii na kiuchumi;
4. Kuendelea kuyaimarisha Mabaraza ya Vijana kwa kufanya mikutano kwa mujibu wa Sheria;
5. Kuimarisha upatikanaji wa huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wa Taasisi zinazotekeleza programu hii; na
6. Kuanzisha vituo viwili vya Vijana (Youth

Development Centre) vitakavyosaidia vijana kupata huduma mbali mbali Unguja na Pemba.

149. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ya Maendeleo ya Vijana iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 7,045,799,000/=**. Kati ya hizo **Shilingi 645,799,000/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 6,400,000,000/=** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Programu Kuu PJ0303: Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (Tzs 15,840,971,000/=)**.

150. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa utamaduni, Lugha ya Kiswahili na Sanaa ya Zanzibar inawaendeleza wasanii kiuchumi ili kupunguza umasikini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa na uhifadhi wa utamaduni, Kukua kwa michezo na miundombinu yenye viwango vya kimataifa, kuongezeka medali kupitia mashindano mbali mbali ya michezo, kuimarika afya za wananchi, kuwa na umoja na mshikamano nchini. Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu ndogo: Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu; na

ii. Programu ndogo: Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo.

**151. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kusimamia, kuhamasisha, kukuza, kuendeleza na kutoa elimu kuhusiana na matumizi bora ya lugha ya Kiswahili na lahaja zilizopo ndani na nje ya nchi;
2. Kuviimarisha na kuvijengea uwezo vikundi vya sanaa vya Taifa pamoja na kuvisaidia vikundi vya Sanaa vya Wilaya na Shehia;
3. Kusajili, kusimamia, kukagua na kudhibiti kazi na haki za wasanii na wabunifu wa kazi za sanaa pamoja na kuwapatia mirabaha yao;
4. Kufanya ukarabati wa studio ya Sanaa Rahaleo na kujenga Nyumba ya Sanaa;
5. Kuendeleza michezo kwa kuziwezesha timu kushiriki na kuandaa mashindano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na kuvisaidia vyama vya michezo;
6. Kuendeleza miundombinu ya michezo kwa kufanya ukarabati wa kiwanja cha Amani, Gombani, Mao- Zedong; Kuviboresha viwanja vya Wilaya na Kujenga viwanja vidogo vidogo vya (4in1)
7. Kuandaa mafunzo ya Kitaifa na Kimataifa kwa

waamuzi, makocha, viongozi na wanamichezo pamoja na kuandaa bonanza siku ya mazoezi ya viungo;

8. Kuimarisha huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa taasisi zinazotekeleza programu hii; na
9. Kujenga miundombinu ya michezo ikiwemo Bwawa la kuogelea (swiming pool) la kisasa lenye viwango vya kimataifa na Akademia ya Michezo (Sports Academy).

**152.** **Mheshimiwa Spika,** ili programu ya Maendeleo ya Utamaduni na Michezo iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 15,840,971,000/=**. Kati ya hizo **Shilingi 3,840,971,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 12,000,000,000/=** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Programu Kuu PJ0304: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (Tshs 3,215,030,000/=)**

**153.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na kuratibu na kusimamia Utawala na Uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara.

Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa usimamizi bora wa mipango na uendeshaji wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii itakuwa na Programu ndogo tatu zifuatazo:-

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara;
ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; na
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

154. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

1. Kukamilisha mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Wizara na Taasisi zilizomo chini ya Wizara;
2. Kuratibu na kusimamia utafiti ;
3. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara;
4. Kutayarisha bajeti na taarifa za utekelezaji pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa miradi, programu na shughuli za Wizara;
5. Kuendelea kuratibu vikao vya ushirikiano vya SMT na SMZ kwa Wizara na Taasisi zilizomo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo;
6. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa

kuwapatia vifaa, huduma muhimu pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao;

7. Kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya masuala mtambuka ikiwemo udhalilishaji, Ukimwi, na mikakati ya kupambana na rushwa Zanzibar;
8. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa mujibu wa kada zao ili kufanya kazi kwa ufanisi pamoja na kufanya upimaji kwa wafanyakazi hao kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi zao;
9. Kuratibu shughuli na ziara za kikazi za viongozi Kitaifa na Kimataifa; na
10. Kuratibu na Kusimamia shughuli zote za Wizara kwa Upande wa Pemba.

**155. Mheshimiwa Spika,** ili programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 3,215,030,000/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**156. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023,

naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo zenye jumla ya **Shilingi 49,081,861,000/=**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,344,600,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 32,737,261,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazo tumika kwa kila Programu umeainishwa kwenye. **(Kiambatanisho namba 1G kinahusika )**.

**157. Mheshimiwa Spika,** matarajio ya upatikanaji wa fedha hizi kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo itapelekea kutimiza Malengo yake katika maeneo yafuatayo:

1. Wananchi kupata taarifa mbali mbali za utekelezaji wa shughuli za Serikali na Kukuza taswira ya Mheshimiwa Rais na Wasaidizi wake;
2. Taasisi za habari kuwa na uwezo wa kiutendaji na vifaa vya kisasa vya habari na kutumia TEHAMA kwenye sekta ya habari na mawasiliano kwa umma;
3. Ustawi wa huduma za Bohari na Uchapaji kwa Taasisi za Serikali na Binafsi;
4. Vijana kuwa na uelewa wa mambo yanayowahusu wao na kuongezeka kwa ajira za vijana;

5. Wananchi kufuata Utamaduni wa Mzanzibari na kujiajiri kupitia sanaa na Michezo;
6. Kuwepo kwa Miundombinu yenye viwango vinavyokubalika kimataifa, kupata medali nyingi kwa kushiriki mashindano mbali mbali ya michezo, kuwa na afya nzuri, kuwa na amani pamoja na kuendeleza umoja na ushirikiano miongoni mwa wananchi kupitia Sanaa na Michezo;
7. Kusimamia utekelezaji wa maagizo na ahadi za Mheshimiwa Rais; na
8. Kusimamia na Kutathmini Mipango ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

## I. HITIMISHO

158. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena naomba kumpongeza na kumshukuru **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa umahiri katika kuiongoza nchi yetu vyema. Umahiri na umakini alionao umechangia kwa kiasi kikubwa sana katika kudumisha amani na utulivu tulio nao. Vile vile, naomba nimpongeze tena Mheshimiwa Rais kwa juhudi mbali mbali anazoendelea kuchukuwa katika kuhakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 inatekelezwa kikamilifu.

**159. Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu kuwa nchi yetu inategemea kufanya Sensa ya Watu na Makazi ifikapo mwezi Agosti 2022. Wizara yangu ikiwa kama mdau mkubwa wa Sensa nachukua fursa hii kuwaomba wananchi wote kujitokeza kwa wingi kuhesabiwa ili waisaidie Serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, mageuzi ya masuala ya Afya, Elimu pamoja na kwenda sambamba na ajenda za maendeleo za kimataifa.

**160. Mheshimiwa Spika,** pongezi zangu za dhati nazipeleka kwa watendaji wote wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Nikianza na Katibu Mkuu Ndugu. Fatma Hamad Rajab, Naibu Katibu Mkuu Ndugu. Khamis Abdulla Said, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Makamishna, Makatibu Watendaji na wafanyakazi wote kwa namna munavyonipa Ushirikiano mkubwa na wepesi wa kuiongoza Wizara hii katika kutimiza Malengo yake.

**161. Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waandishi wa Habari wote, Vijana wote, Wanamichezo, Wasanii na Wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za Wizara yangu. Pia shukurani za pekee ziende kwa Vyombo vya Habari vya Serikali na Binafsi kwa kufanikisha kurusha vipindi mbali mbali vya kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Vijana, Utamaduni na taarifa za michezo.

162. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kuzishukuru Wizara zote za Serikali pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali kwa ushirikiano mzuri mnaotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Wizara.

163. **Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu mkubwa naomba nizishukuru nchi mbali mbali na Mashirika ya kimaendeleo ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Afrika ya Kusini, Ufaransa, Shirika la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), UNICEF, UNESCO, Shirika la Milki Bunifu Ulimwenguni (WIPO), ARIPO, PBZ, CRDB, NMB, Equity Bank, NIC, ZAT, BANDARI, ZURA, SUZA, AZAM Media, Coaches Across Continents, KOICA, Youth Challenge International, TAMWA, JUWAHAZA, TAHA, S.O.S, CHARITY SCHOOL BWEJUU, Tume ya Utangazaji Tanzania, Jukwaa la Wahariri, Baraza la Habari, Asasi za Kiraia zinazosaidia Vijana pamoja na Washirika wote wa Maendeleo tulioshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

164. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa kuniskiliza kwa makini wakati wote wa kuwasilisha hotuba hii. Ni matumaini yangu kuwa mtatoa ushauri na michango mizuri itakayosaidia utekelezaji wa majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa.

165. **Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza kusoma hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo naomba kuchukuwa fursa hii kukushukuruni sana kwa namna ambavyo tumeshirikiana katika kufanikisha majukumu yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu atuondoshee mitihani ya maradhi na atuzidishie neema katika nchi yetu.

166. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu liipokee, liijadili na kutushauri na hatimae liipitishe Bajeti hii.

167. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita (MBM),**
**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**
**Zanzibar.**

# VIAMBATANISHO

| KIAMBATISHO NAMBA 1 A | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | | | | |
| **NO** | **IDARA** | **MAELEZO** | **BAJETI (2021/2022)** | **FEDHA ZILIZOPATIKA NA JULY - MARCH 2021/2022** | **ASILI MIA** |
| **1** | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 673,110,040 | 498,086,020 | 74% |
| | | Matumizi Mengineo | 250,000,000 | 115,000,000 | 46% |
| | ***JUMLA*** | | ***923,110,040*** | ***613,086,020*** | ***66%*** |
| **2** | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 0 | 0 | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 155,600,000 | 44,000,000 | 28% |
| | ***JUMLA*** | | ***155,600,000*** | ***44,000,000*** | ***28%*** |
| **3** | Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 960,620,840 | 770,729,350 | 80% |
| | | Matumizi Mengineo | 630,000,000 | 289,319,500 | 46% |
| | ***JUMLA*** | | ***1,590,620,840*** | ***1,060,048,850*** | ***67%*** |
| **4** | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 158,351,400 | 113,209,620 | 71% |
| | | Matumizi Mengineo | 140,000,000 | 84,985,000 | 61% |
| | **JUMLA** | | **298,351,400** | **198,194,620** | **66%** |
| **5** | Idara ya Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 1,649,088,240 | 1,245,872,005 | 76% |
| | | Matumizi Mengineo | 317,760,000 | 105,055,500 | 33% |
| | **JUMLA** | | **1,966,848,240** | **1,350,927,505** | **69%** |
| **6** | Idara ya Michezo | Mishahara | 0 | 0 | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 300,000,000 | 98,645,000 | 33% |
| | **JUMLA** | | **300,000,000** | **37,000,000** | **12%** |
| **7** | Idara ya Habari (Maelezo) | Mishahara | 420,629,480 | 329,646,865 | 78% |
| | | Matumizi Mengineo | 360,640,000 | 65,580,000 | 18% |
| | **JUMLA** | | **781,269,480** | **395,226,865** | **51%** |
| | ***Jumla ya Mishahara*** | | ***3,861,800,000*** | ***2,957,543,860*** | ***77%*** |
| | ***Jumla ya Matumizi Mengine*** | | ***2,154,000,000*** | ***802,585,000*** | ***37%*** |
| | **Jumla Kuu kwa Taasisi zisizopokea Ruzuku** | | **6,015,800,000** | **3,760,128,860** | **63%** |

***Taasisi za Ruzuku***

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **Baraza la Vijana Zanzibar** | **Mishahara** | **0** | **0** | **0** |
| | | Matumizi Mengineo | 238,800,000 | 73,000,000 | 31% |
| | | | **238,800,000** | **73,000,000** | **31%** |
| **2** | Afisi ya Msajili na Hakimiliki | Mishahara | 214,401,660 | 145,311,335 | 68% |
| | | Matumizi Mengineo | 403,300,000 | 135,000,000 | 33% |
| | **JUMLA** | | **617,701,660** | **280,311,335** | **45%** |
| **3** | Baraza la Kiswahili | Mishahara | 0 | 0 | 0 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Zanzibar | Matumizi Mengineo | 248,992,000 | 90,000,000 | 36% |
| | **JUMLA** | | **248,992,000** | **90,000,000** | **36%** |
| **4** | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar | Mishahara | 0 | 0 | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 200,208,000 | 59,069,600 | 30% |
| | **JUMLA** | | **200,208,000** | **59,069,600** | **30%** |
| **5** | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | 0 | 0 | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 161,900,000 | 76,830,000 | 47% |
| | **JUMLA** | | **161,900,000** | **76,830,000** | **47%** |
| **6** | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 250,000,000 | 171,990,195 | 69% |
| | | Matumizi Mengineo | 152,800,000 | 112,291,000 | 73% |
| | **JUMLA** | | **402,800,000** | **284,281,195** | **71%** |
| **7** | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 2,325,798,340 | 1,629,331,275 | 70% |
| | | Matumizi Mengineo | 2,058,900,000 | 230,000,000 | 11% |
| | **JUMLA** | | **4,384,698,340** | **1,859,331,275** | **42%** |
| **8** | Shirika la Magazeti | Mishahara | 543,400,000 | 383,308,410 | 71% |
| | | Matumizi Mengineo | 112,300,000 | 114,000,000 | 102% |
| | **JUMLA** | | **655,700,000** | **497,308,410** | **76%** |
| **9** | Kampuni ya Uunganisha Maudhui (ZMUX) | Mishahara | 0 | 0 | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 393,400,000 | 75,000,000 | 19% |
| | **JUMLA** | | **393,400,000** | **75,000,000** | **19%** |
| **10** | Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP) | Mishahara | 1,104,100,000 | 862,632,740 | 78% |
| | | Matumizi Mengineo | 0 | 0 | 0 |
| | **JUMLA** | | **1,104,100,000** | **862,632,740** | **78%** |
| | Jumla ya Mishahara ya Ruzuku | | 4,437,700,000 | 3,192,573,955 | 72% |
| | Jumla ya matumizi mengineo ya ruzuku | | 3,970,600,000 | 965,190,600 | 24% |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **8,408,300,000** | **4,157,764,555** | **49%** |
| | Jumla ya Mishahara kwa Wizara | | 8,299,500,000 | 6,150,117,815 | 74% |
| | Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara | | 6,124,600,000 | 1,767,775,600 | 29% |
| | **Jumla kuu ya wizara matumizi ya kawaida (A)** | | **14,424,100,000** | **7,917,893,415** | **55%** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **B: Miradi ya Maendeleo** | | | |
| **1** | Mradi wa Maendeleo ya Vijana | 7,000,000,000 | 0 | 0% |
| **2** | Uimarishaji wa viwanja vya Wilaya SMZ | 4,000,000,000 | 121,000,000 | 3% |
| **3** | Ujenzi wa Viwanja vya Nje na Academy | 3,000,000,000 | 0 | 0% |
| **4** | Programu ya Uimarishaji Utowaji Matangazo | 19,201,500,000 | 668,000,000 | 3% |
| **5** | Ununuzi wa Mtambo wa Kuchapia Magazeti | 13,747,481,000 | 0 | 0% |
| **6** | Ununuzi wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji | 9,520,000,000 | 0 | 0% |
| | **Jumla Kuu ya Wizara Miradi ya Maendeleo (B)** | **56,468,981,000** | **789,000,000** | **1%** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)** | **70,893,081,000** | **8,706,893,415** | **12%** |

**KIAMBATANISHO 1B**

**MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2021 HADI MACHI 2022**

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| ***NO*** | ***TAASISI*** | ***BAJETI 2021/2022*** | ***FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022*** | ***ASILIMIA*** |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 300,000,000 | 127,575,946 | 43% |
| **2** | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 14,200,000 | 6,469,000 | 46% |
| **3** | Habari Maelezo | 300,000,000 | 48,947,750 | 16% |
| **4** | Tume ya Utangazaji | 440,000,000 | 152,197,329 | 35% |
| **5** | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 250,026,000 | 100,487,394 | 40% |
| **6** | Ofisi kuu Pemba | 80,000,000 | 29,078,000 | 36% |
| | **JUMLA** | **1,384,226,000** | **464,755,419** | **34%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1C**

**MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA**

| **NO.** | **TAASISI** | **BAJETI 2021/2022** | **MAPATO YALIKUSANYWA JULAI 2021 HADI MACHI 2022** | **SILIMIA** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 1,200,000,000 | 686,045,163 | **57%** |
| 2 | Shirika la Magazeti | 1,011,900,000 | 665,154,791 | **66%** |
| 3 | ZAGPA | 4,362,830,890 | 1,631,520,403 | **37%** |
| 4 | ZMUX | 1,500,000,000 | 1,007,089,519 | **67%** |
| | **JUMLA** | **8,074,730,890** | **3,989,809,876** | **49%** |

## KIAMBATISHO NAMBA 1D

## FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

**Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Habari Maelezo | 781,269,480 | 395,226,865 | 51% |
| 2 | Shirika la Utangazaji ZBC | 4,384,698,340 | 1,859,331,275 | 42% |
| 3 | Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX) | 393,400,000 | 75,000,000 | 19% |
| 4 | Shirika la Magazeti ya Serikali | 655,700,000 | 497,308,410 | 76% |
| 5 | Programu ya Uimarishaji Utowaji Matangazo | 19,201,500,000 | 0 | 0% |
| | **JUMLA** | **25,324,165,000** | **3,494,866,550** | **14%** |

**Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapishaji**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tume ya Utangazaji | 402,800,000 | 284,281,195 | 71% |
| 2 | Wakala ya SMZ wa Uchapaji (ZGP) | 1,104,100,000 | 862,632,740 | 78% |
| 3 | Ununuzi wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji | 9,520,000,000 | 0 | 0% |
| 4 | Ununuzi wa Mtambo wa Kuchapia Magazeti | 13,747,481,000 | 668,000,000 | 3% |
| | **JUMLA** | **24,795,441,000** | **1,146,913,935** | **5%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu Pemba | 923,110,040 | 613,086,020 | 66% |
| | **JUMLA** | **923,110,040** | **613,086,020** | **66%** |

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Maendeleo ya Vijana | 298,351,400 | 198,194,620 | 66% |
| 2 | Baraza la Vijana Zanzibar | 238,800,000 | 73,000,000 | 31% |
| | **JUMLA** | **538,151,400** | **271,194,620** | **50%** |
| 3 | Programu ya Ajira kwa Vijana | 7,000,000,000 | 0 | 0% |
| | **JUMLA** | **7,538,151,400** | **271,194,620** | **4%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2021/2022 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utamaduni na Sanaa | 1,966,848,240 | 1,350,927,505 | 69% |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **2** | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 200,208,000 | 59,069,600 | 30% |
| **3** | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 248,992,000 | 90,000,000 | 36% |
| 4 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 617,701,660 | 280,311,335 | 45% |
| | **JUMLA** | **3,033,749,900** | **1,780,308,440** | **59%** |

| **Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NO.** | **TAASISI** | **BAJETI 2021/2022** | **FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022** | **ASILIMIA** |
| 1 | Idara ya Michezo | 300,000,000 | 98,645,000 | 33% |
| 2 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | 161,900,000 | 76,830,000 | 47% |
| 3 | Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo pamoja na ujezi wa Academy | 7,000,000,000 | 121,000,000 | 2% |
| | **JUMLA** | **7,461,900,000** | **296,475,000** | **4%** |
| **Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni na Michezo** | | | | |
| **NO.** | **TAASISI** | **BAJETI 2021/2022** | **FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADIMACHI 2022** | **ASILIMIA** |
| 1 | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,590,620,840 | 1,060,048,850 | 67% |
| | **JUMLA** | **1,590,620,840** | **1,060,048,850** | **67%** |
| **Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara** | | | | |
| **NO.** | **TAASISI** | **BAJETI 2021/2022** | **FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022** | **ASILIMIA** |
| 1 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 155,600,000 | 44,000,000 | 28% |
| | **JUMLA** | **155,600,000** | **25,000,000** | **16%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1E**

**FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapishaji**

| NO | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Habari Maelezo | 300,000,000 | 48,947,750 | 16% |
| 3 | Shirika la Magazeti | 1,011,900,000 | 665,154,791 | 66% |
| 4 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 1,200,000,000 | 686,045,163 | 57% |
| 6 | Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) | 1,500,000,000 | 1,007,089,519 | 67% |
| | **JUMLA** | **4,011,900,000** | **2,407,237,223** | **60%** |

**Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari**

| NO | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tume ya Utangazaji | 440,000,000 | 152,197,329 | 35% |
| 2 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP) | 4,362,830,890 | 1,631,520,403 | 37% |
| | **JUMLA** | **4,802,830,890** | **1,783,717,732** | **37%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi kuu Pemba | 80,000,000 | 29,078,000 | 36% |
| | **JUMLA** | **80,000,000** | **29,078,000** | **36%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 300,000,000 | 127,575,946 | 43% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 14,200,000 | 6,469,000 | 46% |
| 3 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 250,026,000 | 100,487,394 | 40% |
| | **JUMLA** | **564,226,000** | **234,532,340** | **42%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2021 HADI MACHI 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 300,000,000 | 127,575,946 | 43% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 14,200,000 | 6,469,000 | 46% |
| 3 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 250,026,000 | 100,487,394 | 40% |
| | **JUMLA** | **564,226,000** | **234,532,340** | **42%** |

**KIAMBATANISHO 1F**
**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**
**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

**A: MATUMIZI**

| No | IDARA | MAELEZO | BAJETI 2021/2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 657,230,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 260,000,000 |
| ***JUMLA*** | | | **917,230,000** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 160,800,000 |
| ***JUMLA*** | | | **160,800,000** |
| 3 | Uendeshaji na utumishi | Mishahara | 1,027,000,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 1,110,000,000 |
| ***JUMLA*** | | | **2,137,000,000** |
| 4 | Habari Maelezo | Mishahara | 462,500,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 510,000,000 |
| ***JUMLA*** | | | **972,500,000** |
| 5 | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 148,899,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 145,000,000 |
| ***JUMLA*** | | | **293,899,000** |
| 6 | Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 1,728,471,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 445,000,000 |
| ***JUMLA*** | | | **2,173,471,000** |
| 7 | Michezo | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 310,000,000 |
| ***JUMLA*** | | | **310,000,000** |
| ***Jumla ya Mishahara*** | | | **4,024,100,000** |
| ***Jumla ya Matumizi mengine*** | | | **2,940,800,000** |
| ***Jumla Kuu kwa taasisi zisizopokea Ruzuku*** | | | **6,964,900,000** |
| | | | |
| | | ***TAASISI ZA RUZUKU*** | |
| 1 | Shirika la Magazeti ya Serikali | Mishahara | 557,600,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 726,100,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***1,283,700,000*** |
| 2 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 2,173,800,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 2,203,000,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***4,376,800,000*** |
| 3 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | Mishahara | 1,204,500,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 0 |
| | ***JUMLA*** | | ***1,204,500,000*** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| *4* | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 220,800,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 163,500,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***384,300,000*** |
| *5* | Kampuni ya Unganishaji Maudhui (ZMUX) | Mishahara | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 421,000,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***421,000,000*** |
| *6* | Baraza la Vijana | Mishahara | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 351,900,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***351,900,000*** |
| *7* | Afisi ya Msajili Hakimiliki | Mishahara | 204,200,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 431,600,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***635,800,000*** |
| *8* | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 303,900,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***303,900,000*** |
| *9* | Baraza la Sanaa,Sensa ya filamu na Utamaduni | Mishahara | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 244,600,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***244,600,000*** |
| *10* | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | 0 |
| | | Matumizi Mengineo | 173,200,000 |
| | ***JUMLA*** | | ***173,200,000*** |
| | | | |
| | ***Jumla ya Mishahara Ruzuku*** | | ***4,360,900,000*** |
| | ***Jumla ya matumizi mengineo ruzuku*** | | ***5,018,800,000*** |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **9,379,700,000** |
| | | | |
| | ***Jumla ya Mishahara kwa Wizara*** | | ***8,385,000,000*** |
| | ***Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara*** | | ***7,959,600,000*** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (Matumizi ya kawaida) A** | | **16,344,600,000** |

**B: Miradi ya Maendeleo**

| | | |
|---|---|---|
| | **Mradi wa Maendeleo ya Vijana** | **6,400,000,000** |
| 1. | Uimarishaji wa viwanja vya Wilaya SMZ | 4,000,000,000 |
| 2. | Bwawa, Viwanja vya (4 in 1) na Academy | 3,000,000,000 |
| 3. | Programu ya Uimarishaji Matangazo ZBC | 12,337,261,000 |
| 4. | Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa | 5,000,000,000 |
| 5. | Ununuzi wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji | 2,000,000,000 |
| | **Jumla ya miradi ya maendeleo B** | **32,737,261,000** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (A + B)** | **49,081,861,000** |

## KIAMBATISHO NAMBA 1G

**BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Maendeleo Vijana | 293,899,000 |
| 2 | Baraza la Vijana Zanzibar | 351,900,000 |
| 3 | Programu ya Ajira kwa Vijana | 6,400,000,000 |
| | **JUMLA** | **7,045,799,000** |

**Programu Ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utamaduni na Sanaa na Michezo | 2,173,471,000 |
| 2 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 244,600,000 |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 303,900,000 |
| 4 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 635,800,000 |
| 5 | Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa | 5,000,000,000 |
| | **JUMLA** | **8,357,771,000** |

**Programu Ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 310,000,000 |
| 2 | Baraza la Michezo | 173,200,000 |
| 3 | Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja na Ujenzi wa Academy | 7,000,000,000 |
| | **JUMLA** | **7,483,200,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| **1** | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 160,800,000 |
| | **JUMLA** | **160,800,000** |

**Programu Ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| **1** | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 2,137,000,000 |
| | **JUMLA** | **2,137,000,000** |

**Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji Zanzibar | 16,714,061,000 |
| 2 | Idara ya Habari Maelezo | 934,785,000 |
| 3 | Shirika la Magazeti | 1,283,700,000 |
| 5 | Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) | 421,000,000 |
| | **JUMLA** | **19,353,546,000** |

**Programu Ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Tume ya Utangazaji | 384,300,000 |
| 2 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 3,204,500,000 |
| 3 | Idara ya Habari Maelezo | 37,715,000 |
| | **JUMLA** | **3,626,515,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 MATUMIZI |
|---|---|---|
| | Ofisi Kuu Pemba | 917,230,000 |
| | **JUMLA** | **917,230,000** |

**KIAMBATISHI NAMBA 1H**
**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**
**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO | TAASISI | BAJETI 2022/2023 |
|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 260,000,000 |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 25,000,000 |
| 3 | Habari Maelezo | 120,000,000 |
| 4 | Tume ya Utangazaji | 300,000,000 |
| 5 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 81,000,000 |
| 6 | Ofisi Kuu Pemba | 89,997,000 |
| | **JUMLA** | **875,997,000** |

**KIAMBATANISHO 1J**
**MAPATO YATAKAYO KUSANYWA NA YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA**

| NO | TAASISI | MAKUSANYO |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 1,400,000,000 |
| 2 | Shirika la Magazeti | 1,011,900,000 |
| 3 | ZAGPA | 4,700,000,000 |
| 4 | ZMUX | 1,500,000,000 |
| | **JUMLA** | **8,611,900,000** |

**Kiambatanisho Nam .2 Vikundi na Taasisi zilizosaidiwa vifaa na fedha taslimu Unguja na Pemba**

| S/N | JINA LA KIKUNDI | VIFAA |
|---|---|---|
| 1. | Baraza la Vijana Michikichini - Unguja | Bero 3 na Gloves 10 |
| 2. | Perspective Development Skills (PDS) | Vyarahani 3 |
| 3. | Mikunguni Youth Development Organization (MYDO) - Unguja | Viti vya Plas |
| 4. | Mkulima wa Mapeshen - Unguja | Posi 30 za kupandia Mipeshen |
| 5. | Kilimo Fursa Bambi - Unguja | Mipira ya Maji roli 4 |
| 6. | Botanic Garde - Unguja | 200,000/ = kwa ajili ya Chakula cha Kuku |
| 7. | Tuonane Jendele - Unguja | Roli 2 za Maji |
| 8. | Kati FM - Unguja | Redio Recorder 1 |
| 9. | Kitanga Chekundu - Unguja | Shilingi 220,000 /- kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Samaki |
| 10 | Inua Vijana naTehama - Unguja | 300,000/= kwa ajili ya ununuzi wa Canera |
| 11 | Kituo cha Huduma Rafiki cha Vijana - Magirisi - Unguja | Computer na Printer 1 |
| 12 | Msanii chipukizi wa Zenj Flovour - Unguja | 200,000/= kwa ajili ya kurikodi nyimbo |
| 13 | Tujitume Wete Pemba | 200,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Banda la Kuku. |
| 14. | Zindukeni Uwandani - Pemba | 100,000/= kwa ajili ya mbegu na Pembejeo za Kilimo |
| 15. | Zetu ni Ajira zetu cha Tumbe - Pemba | Kupitia Ufadhili wa SOS walipatiwa mashine 2 za Boti |
| 16 | Uvumilivu Group cha Vitongoji - Pemba | Kupitia ufadhili wa SOS walipatiwa Friza |
| 17 | Atoae ni Mungu cha Dodo - Pemba | Kupitia ufadhili wa SOS walipatiwa mashine 1 ya Boti. |
| 18 | Riziki Haina Mja – Mjini Ole - Pemba | 1000,000/= kwa ajili ya Ujenzi wa Banda la Kuku. |
| 19. | Mlindo Tundauwa - Pemba | 400,000/= Kwa ajili ya Kufunga mashine ya kusagia. |